# Nipashe

Jumatatu Septemba 21, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580345

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## Wazazi mbaroni madai ya kuoza mwanafunzi

UKURASA 5


Nipashe Spotika

ISIKUPITE

NYOTA WAS WANAOTARAJIWA MAKUBWA EPL MSIMU HUU

UKURASA 11

# Wagombea wazidi kuchanja mbuga

• **Lissu** aahidi mabadiliko, Sendiga wa ADC kutibu umaskini, Maalim Seif kuifanya Zanzibar Singapore, Mwinyi ajira kwa vijana... *Endelea ukurasa 2 & 3*

RIPOTI MAALUM

## Simba 20 hufa kila mwaka kwa kuwekewa sumu kwenye mizoga

UKURASA 4

## Magufuli awapa kibano mawaziri 3

UKURASA 2



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azan Zungu, akipanda mti ikiwa ishara ya kuzindua kampeni ya Pendezesha Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais na Benki ya CRDB Plc iliyofanyika Shule ya Sekondari Goba jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Selemani Jafo, akimkabidhi cheti cha tuzo mmoja wa wahitimu waliosoma nje ya nchi kutokana na kufanya vizuri kwenye mitihani yake ya mwisho. Mahafali hayo yaliandaliwa na Global Education Link (GEL), mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM awapa kibano mawaziri watatu

**Na Gwamaka Alipipi,** TABORA

RAIS John Magufuli ametoa maagizo kwa mawaziri watatu, kutatua kero za wakazi wa Wilaya ya Uvinza, ambazo ni umeme kufika vijijini, kiwanda cha chumvi kuuza bidhaa kimataifa, pamoja na fedha za ukarabati wa barabara kutolewa ndani ya wiki mbili.

Alitoa maagizo hayo jana kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo.

Akiwa wilayani Uvinza njiani kuelekea mkoani Tabora, Rais Magufuli alisikitishwa na hatua ya vijiji 61 vilivyopo wilayani humo kutofikiwa na huduma ya umeme, huku vijiji 17 pekee vikiwa ndivyo vimefikiwa na nishati hiyo.

Kutokana na hali hiyo alimwagiza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kumweleza Waziri wa Nishati, Dk. Kalemani, vijiji hivyo 61 vinafikiwa na umeme haraka.

"Najua suala la umeme katika Wilaya ya Uvinza hatujafanya vizuri kabisa, haiwezekani miaka mitano tuwe tumepeleka umeme katika vijiji 17 tu, najua Waziri wa Nishati ananisikia. DC (Mkuu wa Wilaya) upo hapa. Nataka umeme ufike katika vijiji hivyo. Haiwezekani tuwe tumepeleka umeme katika vijiji zaidi ya 9,000 nchi nzima, halafu vitushinde hivi vichache," alisema Rais Magufuli.

Kadhalika, Rais Magufuli alimwagiza Waziri wa Viwanda na Biashara, Bashungwa, kiwanda cha chumvi cha Uvinza, kinaongeza uzalishaji na kuuza bidhaa hiyo katika nchi za Burundi, pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Hapa Uvinza kuna kiwanda cha chumvi, tunatarajia kukikuza ili kianze kuuza chumvi katika nchi za jirani, pamoja na vijana wetu wapate ajira. Sasa Waziri wa Viwanda angalia suala hili". Pia, aliwahakikishia wananchi wa Wilaya ya Uvinza kuwajengea barabara yenye urefu wa kilometa 10 kwa gharama ya Sh. bilioni tano.

Katika kutimiza ahadi hiyo, Rais Magufuli alilazimika kumpigia simu Waziri wa TAMISEMI, Jafo aidhinishe fedha za ujenzi wa barabara hiyo ndani ya wiki mbili, na mkandarasi aanze kufanya kazi haraka.

Sehemu ya mazungumzo kati ya Rais Magufuli na Waziri Jafo ilikuwa hivi:

**JPM: Waziri Jafo uko wapi?**

**Jafo:** Nipo jimboni mheshimiwa Rais kwenye kampeni.

**JPM:** Nipo Uvinza, kuna barabara ya Uvinza kilometa 10 inahitaji ukarabati, sasa nataka uidhinishe fedha kwa ajili ya ujenzi wake haraka, ndani ya wiki mbili na mkandarasi aanze kazi haraka.

**Jafo:** Nimekusikia Mheshimiwa Rais na nitatekeleza haraka sana, nitahakikisha kiasi hicho cha fedha kinafika kwa wakati na mkandarasi anaanza kazi.

Vile vile, Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano, zaidi ya Sh. bilioni 11.07 zimetumika kukamilisha miradi ya maji katika Wilaya ya Uvinza. Alisema sekta ya elimu zaidi ya Sh. bilioni 6.7 zimetumika kutekeleza sera ya elimu bure. Kadhalika, aliwaahidi wakazi wa Uvinza kuwajengea barabara kutoka Uvinza-Maragalasi (kilometa 51) kiwango cha lami, kwamba zaidi ya Sh. bilioni 51 zimetengwa.

"Tumetengeneza sehemu kubwa ya barabara, hatuwezi kushindwa kilometa 51. Pesa zipo, ndiyo maana nimeamua kupita kwa gari siyo kwa helikopta ili nijue shida mnazopata".

Rais Magufuli alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 26 kwa ajili ya kuunganisha mikoa ya Kagera na Kigoma, na Sh. bilioni 2.18 zitatumika katika Mkoa wa Kigoma ili kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme.

# Lissu aahidi mabadiliko ya kiuchumi, kiutawala

**Na Anthony Kayanda,** KIGOMA

MGOMBEA urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, ameahidi kufanya mabadiliko ya kiuchumi na kiutawala kama atachaguliwa, huku akiwataka wakazi wa Kigoma Mjini kuchagua mgombea yeyote mwenye nguvu ya kuiondoa CCM madarakani katika Jimbo la Kigoma Mjini bila kujali chama.

Aidha, amesema CHADEMA ndicho chama chenye mgombea urais anayeweza kuiondoa CCM madarakani na kuwaomba wananchi kumchagua ili aletea mabadiliko makubwa katika mifumo ya nchi na kuboresha maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Akizungumza na mamia ya wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika eneo la Mwanga mjini Kigoma, aliwataka Watanzania kupiga kura kwa CHADEMA, ili kufikia mabadiliko makubwa ya maisha yao na taifa kwa ujumla.

"Kama mgombea wa CHADEMA katika jimbo hili ana nguvu mchagueni huyo na kama mgombea wa Chama cha ACT-Wazalendo ana nguvu muungeni mkono, yeyote mwenye nguvu ndio mgombea wangu," alifafanua katika jimbo hilo ambalo mgombea wa ACT-Wazalendo ni Zitto Kabwe.

Alisema lengo ni kuitoa CCM madarakani ili CHADEMA iongoze nchi na inatarajia kuleta maendeleo kwa kufuata mfumo wa majimbo ambao unatumika katika baadhi ya nchi zilizoendelea duniani kama Marekani na Kenya.

Lissu alisema iwapo atashinda urais wa Tanzania, atakuwa wa tofauti na marais wote waliopota katika awamu tano, kwa kuwa atafanya mabadiliko ya mfumo wa utawala kupitia mabadiliko ya Katiba inayoendana na mazingira ya sasa ya nchi, ikiwamo kupunguza mamlaka ya rais ambaye kikatiba ana mamlaka kubwa sana na ambayo anaweza kuitumia vibaya.

Kwa mujibu wa Lissu, mabadiliko ya katiba yatahusisha ibara kandamizi dhidi ya uhuru na haki za Watanzania, ikiwamo kufanya mabadiliko ya sheria kandamizi ambazo zimekuwa kikwazo na chanzo cha maumivu kwa wananchi.

"Viongozi wote hawa wameongoza nchi kwa kutumia Katiba ya mwaka 1977 iliyotungwa baada ya Tanganyika kupata uhuru na ndio chanzo cha mateso wanayopata wananchi, lazima tuandike Katiba mpya ili tuondokane na udikteta wa marais wasio waadilifu," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, ili atekeleze majukumu yake ameahidi kufanya mabadiliko ya katiba kwa kupeleka muswada wa mabadiliko bungeni ndani ya siku 100 za kwanza baada ya kuapishwa kwake.

Naye Ally Bananga akizungumza kabla ya kumkaribisha Lissu, alisema mwaka huu CHADEMA haitakubali kura zake kuibwa na mtu yeyote, bali mshindi apatikane kwa haki.

"Kwa sasa unyonge, kuonewa na kuibiwa kura hawakubaliani navyo na wako tayari kujilinda kwa kutumia nguvu ya umma ili kulinda ushindi wa wagombea wa chama hicho," alisema.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kigoma Mjini, Omary Gindi, alisema wananchi wachague wagombea wa CHADEMA ili watekeleze ilani ya chama iliyojikita kwenye haki, uhuru na maendeleo ya watu.

# Sendiga ataja sababu za kugombea urais

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, amesema moja ya sababu iliyomsukuma kugombea kiti hicho ni umaskini uliokithiri hususani maeneo ya vijijini, na kwamba kama atapata ridhaa ya wananchi ya kuwa rais atahakikisha anaondoa matatizo yanayowakabili wananchi na kukwamisha uchumi kukua katika maeneo hayo.

Akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Tanga katika mkutano wa kampeni jana kwenye viwanja vya Negero wilayani Kilindi, mgombea huyo alisema mkoa wa Tanga ni miongoni mwa mikoa maskini na iliyosahaulika kimaendeleo kunakosababishwa na baadhi ya viongozi kutoupa kipaumbele kwenye miradi ya maendeleo.

Alisema akiingia madarakani, jambo kubwa litakuwa ni kuboresha miundombinu hususani ya barabara, maji, elimu na afya ili kufungua mzunguko wa uchumi.

"Mimi nimezaliwa mkoa wa Tanga Wilaya ya Handeni, lakini mkoa wetu ni maskini, ndio maana niliamua kugombea nafasi hii kwa kuwa nina sifa zote za kuwa rais" alisema Sendiga.

Alisema atahakikisha maeneo yote ya vijijini nchini yanakuwa na huduma zote muhimu ikiwamo barabara kwa kuwa uchumi unategemea kilimo na ufugaji.

"Uchumi wetu unategemea kilimo na ufugaji na ndio wananchi tulio wengi tunategemea katika kuendesha maisha yetu, hivyo mimi nitahakikisha maeneo yote yanapitika muda wote iwe masika ama kiangazzi," alisema Sendiga.

Akizungumzia hali ya miundombinu ya barabara wilayani, Sendiga alisema akiwa rais atahakikisha Wilaya ya Kilindi inapata barabara inayounganisha wilaya hiyo na Mkoa wa Manyara inajengwa kwa kiwango cha lami, ili kufungua mzunguko wa uchumi katika mikoa jirani na wilaya hiyo.

Kuhusu kero ya maji, Sendiga alisema kwa muda mrefu wilaya za Kilindi na Handeni zimekuwa na tatizo la upungufu wa maji, hivyo akiingia madarakani atahakikisha anakamilisha mradi wa maji kutoka Mto Pangani uliopita Wilaya Korogwe ili kuweka miundombinu mipya.

"Miundombinu ya maji tunayoitumia hivi sasa imejengwa miaka ya 70, hivyo ni chakavu, haina uwezo wa kuhudumia watu wengi kutokana na ongezeko la watu kuwa kubwa, hivyo mimi nitaweka mabomba mapya na wananchi wetu mtapata maji kwa urahisi," alisema Sendiga.

# Mwinyi kuimarisha utalii kutoa ajira kwa vijana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, amesema ataimarisha sekta ya utalii ili vijana kupata ajira na kuongeza pato la taifa.

Alisema ataboresha maisha ya wajasiriamali, wafanyabiashara wadogo wakiwamo waendesha bodaboda.

Dk. Mwinyi alitoa ahadi hiyo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Aliwataka wananchi kumchagua yeye pamoja na wagombea wote wa CCM, ili kuendeleza kuwaletea naendeleo.

Alieleza kuwa anaimarisha sekta ya viwanda na kuimarisha sekta ya uvuvi.

"Kwa umati huu uliopo hapa leo sina shaka na nina imani mtanipa kura na kushinda katika uchaguzi mkuu," alisema.

Alisema kuwa kazi kubwa serikali imefanya kama miundombinu na huduma za utalii.

"Kuna ambayo hayajafanikiwa, nataka niyashughulikie kama tatizo la maji ambalo naahidi kushughulikia na watu wote wapate maji ikiwamo maeneo ya uwekezaji wa utalii," alisema.

"Kuna tatizo la barabara za lami, sehemu kubwa ya barabara kuu zina lami sasa barabara za ndani za kusafirisha watalii na wenyeji tutahakikisha kazi inamalizika," alisema.

Kuhusu migogoro ya ardhi, alisema ardhi ni rasilimali inayotakiwa kunufaisha wenyeji na wawekezaji kupata haki stahiki.

**SHEIN: URAIS SI WA KUBAHATISHA**

Rais wa Zanzibar na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, amesema nafasi ya urais si ya kubahatisha, bali lazima ishikwe na mtu mwenye sifa za kuhimili maendeleo na ustawi wa nchi kama alivyo mgombea wa CCM Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Dk. Shein aliyasema hayo jana alipokuwa akimnadi Dk. Hussein Mwinyi, katika mkutano huo wa kampeni.

Dk. Shein akikumbushia alipopita Nungwi kuomba kura alipokuwa mgombea urais na kushinda, alisema urais ni nafasi kubwa na nzito ya kuwatumikia wananchi na si ya kufanya majaribio.

Aliwaambia wananchi na wapenzi wa CCM kuwa haoni zaidi ya Dk. Mwinyi haoni mwenye sifa hizo katika orodha ya wagombea wengine.

Dk. Shein alisema "In Shaa Allah Dk. Hussein atapewa na hakuna wa kumpokonya na kuwaomba wananchi wa Zanzibar kumpa kura nyingi mgombea wa urais wa CCM Zanzibar na wagombea wa nafasi nyingine za ubunge, uwakilishi na udiwani.



Mgombea urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akiwapungia mkono wanachama wa CCM wakati alipowasili viwanja vya Mpira Nungwi katika mkutano wa hadhara wa kampeni Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Maalim Seif kuifanya Z'bar kitovu cha uchumi Afrika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia tiketi ya ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema anakusudia kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha uchumi barani Afrika.

Maalim aliyaeleza hayo katika mkutano wake wa kampeni uliofanyika viwanja vya Alabama Michenzani Wilaya ya Mjini Unguja.

Maalim Seif alisema anakusudi kuifanya Zanzibar kuwa na bandari, ambayo wafanyabiashara wataweza kuingiza bidhaa zao bila ya ushuru na wakati wa kutoa watatozwa ushuru kidogo sana.

Alisema akilifanya hilo, wafanyabiashara wa nchi za Afrika Mashariki na Kati wataweza kuingia Zanzibar na kujipatia bidhaa zote wanazozitaka na ushuru utakuwa mdogo.

"Kama jamaa zetu wa Kongo, Burundi, Rwanda, na wengineo wakienda Dubai kufuata bidhaa nina imani wananchi kama mtanichagua watakuja Zanzibar kufuata bidhaa hizo," alieleza Maalim Seif. Alisema anashangazwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushindwa kujenga bandari katika eneo la Mpiga Duru kwa muda wote tangu viongozi walipoeleza.

Alieleza kuwa hivi sasa Bandari ya Malindi haina tena uwezo wa kuhimili meli za makontena.

"Tunakusudia kuijenga bandari ambayo itaweza kubeba zaidi ya meli sita za makontena kwa wakati mmoja," alisema.

Alieleza serikali itakayoongozwa na ACT-Wazalendo inakusudia kujenga bandari ambayo mashirika ya meli za kimataifa yatapata hamu ya kushusha mizigo yao Zanzibar.

"Kwanza tunakusudi kuondoa vikwazo vyote ambavyo vinawafukuza mashirika ya meli au ndege kuja katika nchi yetu, tutashusha kodi ambayo itawafanya waridhike kuja kwetu," alieleza.

Maalim Seif kadhalika aliweka wazi kuwa katika miaka yake mitano atahakikisha Zanzibar inakuwa na shirika lake la ndege ambalo ndege zake zitatembea duniani kote.

Kwa mujibu wa Maalim Seif, yapo makampuni mengi, ambayo yako tayari kuingia ubia na serikali ili kuanzisha shirika hilo.

"Tutakuwa na shirika letu la ndege ambalo tutaliita Zanzibar Airline, hili litasaidia sana kuongeza watalii nchini mwetu," alieleza Maalim Seif ambaye pia ni mwenyekiti wa ACT-Wazalendo. Vilevile, alisema shirika hilo itaisaidia Zanzibar kujitangaza ulimwenguni na watu wengi kupata hamu ya kuingia visiwani humo.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, aliuambia umma kuwa anakusudia kupanga upya uwanja wa ndege wa Zanzibar ili uwe na uwezo wa kubeba ndege nyingi kwa wakati mmoja.

"Nipeni kura zenu halafu muone nitakavyoibadilisha Zanzibar kuwa kama Singapore kwa maendeleo na mwonekano wake kwa ujumla," alibainisha.

Maalim Seif anaendelea na kampeni katika kisiwa cha Unguja, baada ya kukamilisha awamu ya kwanza katika kisiwa cha Pemba.

# Majaliwa: Ilani ya CCM imeanzisha masoko 28 madini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeanzisha masoko 28 ya madini likiwamo la Nyamongo ili kuwainua wachimbaji wadogo ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ya 2015-2020.

Hayo yalibainishwa jana na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Kassim Majaliwa, alipokuwa akizungumza na wakazi wa Nyamongo, Nyamwaga na Tarime Mjini, wilayani Tarime, mkoani Mara alipokuwa akimwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli na wagombea ubunge wa Jimbo la Tarime Mjini, Michael Kembaki, na Tarime Vijijini, Mwita Waitara na wagombea udiwani wa kata zote za wilaya ya Tarime.

"Kupitia mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali za madini, serikali imeanzisha masoko 28 ya madini, vituo vidogo 28 vya ununuzi wa madini na ujenzi wa vituo saba vya mafunzo ya umahiri kwa wachimbaji wadogo vya Bariadi, Musoma, Bukoba, Mpanda, Chunya, Songea na Handeni," alisema.

"Hatua hizi pamoja na kusaidia kuongezeka kwa mapato ya serikali zimesaidia kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini, kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika, kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini, kuondoa tatizo la utoroshaji na biashara haramu ya madini," alisema.

Akiwafafanulia mambo yaliyofanywa na serikali ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ndani ya miaka mitano, Majaliwa alisema baadhi ya kodi kwenye biashara ya madini zenye kero kwa wachimbaji wadogo ikiwamo kodi ya zuio asilimia tano na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) asilimia 18 zimeondolewa.

Akielezea tathmini ya fidia kwa wananchi wa Nyamongo, Majaliwa alisema uthamini kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la maji machafu eneo la Nyamongo kwa vijiji vya Matongo, Nyabichune na Komarera ulianza Julai, 2019 na malipo ya fidia yalianza kutolewa Mei 2020.

"Hadi sasa Sh. bilioni 32.9 zimelipwa kwa wananchi 1,620 na wananchi 13 wamebaki ambao hawajachukua malipo yao yenye thamani ya shilingi milioni 833. Hao 13 wanasubiri kulipwa kwa sababu walisema hawaridhiki na uthamini wa mali zao, kwa hiyo tathmini itafanyika upya na watalipwa fedha zao," alisema Majaliwa.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**EDBP & GD CONSTRUCTION LIMITED** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CARINA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 176 AXH.** Chassis namba **AT2116054470.** Engine namba **7AH352203.** YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MBE/KYE/RB/673071/2020.**

115908102

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**KAZOBA ENGLISH MEDIUM SCTIN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HIACE YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 265 AJE.** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KA **H/TR/RB/325/2020**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**MAKOMANGO PETRO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **M C 293 BYZ** AINA YA SANLG YENYE CHASIS NO **LBRSPJB55J9018859** NA ENGINE **NO SLI57FMII8922214** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KA **H/RB//6112/2020**

# Simba 20 hufa kila mwaka kwa kuwekewa sumu kwenye mizoga

## ■Tanzania yaongoza kwa simba wengi Afrika

**Na Salome Kitomari,**
MANYARA

MTAFITI wa simba katika ikolojia ya Manyara Tarangire, Dk. Bernard Kissui, amesema wastani wa simba 20 huuawa kila mwaka katika eneo hilo kutokana na binadamu kulipiza kisasi kwa kuweka sumu katika mizoga ya wanyama waliouawa na wanyama hao.

Wanyama wengine wakiwamo fisi, bweha na ndege ambao hula mizoga hiyo, nao hufa kwa wingi kutokana na binadamu kulipiza kisasa, jambo linahitaji ushirikiano wa wadau wote kuokoa kupotea kwa wanyama hao muhimu kwa utalii.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na waandishi wa habari kutoka Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), waliokwenda eneo hilo kuandika habari za uhifadhi na ujangili wa wanyamapori chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la watu wa Marekani (USAID Protect), alisema ni lazima hatua zichukuliwe mapema kwa kuwa simba wanazidi kupungua.

Utafiti wao ulibaini kuwa simba wengi wanauawa kutokana na migongano na binadamu, kwa maana ya kula mifugo na binadamu wanaamua kuweka sumu.

Anasema tangu mwaka 2003 wamekuwa wakiwafuatilia simba kwa kuwavisha vifaa maalum na kubaini kuwa wengi wanauawa baada ya kuua mifugo, baadaye wananchi huweka sumu kwenye mizoga ambayo huua wanyama wengine wengi zaidi.

Dk. Kissui ambaye ni Mkurugenzi wa kituo cha masomo ya usimamizi wa wanyamapori cha SFS, anasema idadi ya simba wanaouawa kwa sababu ya kula mifugo inazidi kuongezeka pamoja na wananchi kupoteza mifugo mingi.

Anatoa mfano wa tukio la mwaka 2016 katika kijiji cha Miswakini chini, simba sita waliuawa ikiwa ni ukoo wa mama, baba, kaka, dada na watoto, baada ya mmoja wao kuua ng'ombe na wananchi kwa hasira kuweka sumu na kusababisha familia hiyo kuteketea.

"Miongoni mwa simba waliouawa ni waliowekewa vifaa maalum vya kutambua walipo na mmoja alifungiwa kifaa ndani ya Hifadhi ya Tarangire, lakini aliuawa mwaka 2018 katika kijiji cha Kakoi alipokula ng'ombe na wananchi waliweka sumu kwenye mzoga na baadaye simba wengine wanne walikula mzoga huo na kufa," anabainisha.


Mfano mwingine alioutoa ni wa tukio la mwaka 2009 ambako kulikuwa na ukame na katika kijiji cha Kimotoro Simanjiro, kulikuwa na makundi ya mifugo yanayoingia eneo lililohifadhiwa la Mkungunero na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, simba walikula ng'ombe watano baadaye mizoga iliwekwa simu na kuua simba saba na wanyama wengine.

Dk. Kissui anasema tukio lingine ni la mwaka 2013 simba kula ng'ombe na wananchi wakaweka sumu kwenye mzoga na kusababisha simba mama na watoto wawili kuuawa, na madhara yakaenda kwa ndege aina ya tumbusi zaidi ya 70 na fisi na bweha.

"Ukiua simba saba miongoni mwake kuna mama, baba, kaka na watoto maana yake umeua familia nzima. Tatizo la watu kutumia sumu kwa kulipiza kisasi kwasababu mifugo yao imeliwa linaleta madhara makubwa sana, nia yao ilikuwa kuua simba, lakini wameua wanyama wengine wasiohusika," anasema mtafiti huyo.

Dk. Kissiu anasema matukio yote ya kuuawa kwa simba nje ya hifadhi za taifa yanazidi kuongezeka kutokana na watu kujenga na kuishi katika mapito na maeneo ya mtawanyiko ya wanyama ambao huenda hadi eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na maeneo mengine kwa ajili ya kupata mahitaji muhimu ya maisha yao.

Anasema katika eneo hilo simba na tembo wamewekewa vifaa maalum kwa ajili ya kujua ni maeneo gani wanapita zaidi na kubaini kuwa wengi hupita shoroba kwa Kwachinja na kijiji cha Mswakini chini, ambayo ni muhimu yakafunguliwa ili kuruhusu wanyama kupita.




Mtafiti wa simba katika ikolojia ya Tarangire Manyara, iliyoko mikoa ya Arusha na Manyara, Dk. Bernard Kissui, akionyesha kwenye ramani wanyama wanavyopita kwa wingi katika shoroba ya Kwakuchinja inayounganisha Hifadhi za Taifa ya Tarangire na Ziwa Manyara. Shoroba hiyo inapungua ukubwa kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu. **PICHA: SALOME KITOMARI**

### MATUMIZI YA KAMERA

Anasema waliweka kamera katika maeneo hayo ambazo zimepiga picha kuonyesha uhalisia wa wanyama kupita na kubaini kuwa Burunge WMA ni muhimu kwa uhifadhi kwa kuwa kuna wanyama wengi wanaopita.

Ndani ya siku 3,900 picha 4,035 zimeonyesha kuwa aina ya wanyama 80 wanaopita ndani ya Burunge WMA jambo linaoonyesha eneo hilo linasaidia uhifadhi wa bayonuwai kukua na kukuza utalii wa eneo hilo.

### SIMBA WENGI WABAKIA TANZANIA

Upo uwezekano wa simba kupotea na barani Ulaya hakuna simba huku Asia wakibaki wachache, India pekee, na kwa Afrika zipo nchi wamepotea kabisa ikiwamo Algeria.

Anasema barani Afrika kunakadiriwa kuna simba zaidi ya 30,000 kati yake 15,000 hadi 16,000 wanapatikana Tanzania, huku eneo la Manyara Tarangire mwaka 2003 likiwa na simba zaidi ya 200, lakini kwa sasa wanakadiriwa kubakia 180, hali inayoonyesha wanapungua.

### UMRI WA SIMBA

Mtafiti huyo anasema kuwa simba jike huishi kati ya miaka 15 hadi 16 na dume miaka 10, kutokana na changamoto nyingi na kwamba jike huishi zaidi kutokana na uhakika wa kubakia kwenye familia, lakini dume hufukuzwa na kuanza kujitafutia chakula wakati ameshachoka na hawezi kupigana na dume jingine ili kupata ufalme kwenye familia nyingine.

### UMUHIMU WA SHOROBA

Shoroba ni eneo lililotambuliwa na Sheria Namba 5 ya Wanyamapori na kanuni zake ambalo ni mapito ya wanyama kutoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda jingine, pia wanyama huenda kwenye maeneo ya mtawanyiko kwa ajili ya kupata madini muhimu, chakula na kwa ajili ya kuzaliana.

Utafiti wa mwaka 2009 uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), ulionyesha kuwa ifikapo mwaka 2050 zitabakia shoroba mbili pekee, nyingi zikiwa zimeingiliwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo kusajili vijiji.

### MADHARA SIMBA KUISHI ENEO MOJA

Mtafiti huyo ambaye amefanya kazi hiyo kwa zaidi ya miaka 20, anasema yapo madhara makubwa ya simba na wanyama wengine kuishi katika kisiwa yaani ndani ya hifadhi bila kwenda eneo jingine, na kwamba ni makubwa ambayo yanaweza kupoteza simba wote.

"Kuzuia wanyama wasipite kwenye shoroba kwenda eneo jingine lililohifadhiwa kutasababisha kuzaliana wao kwa wao yaani baba na mtoto, kaka na dada na mwishowe kupata kizazi dhaifu na iwapo ugonjwa utaingia ni rahisi kufa na kupotea," anasema.

"Kama tunataka simba na wanyama wengine waendelee kuwepo ni lazima shoroba zifunguliwe, lazima tuangalie namna ya kujenga miundombinu ya barabara inayoruhusu matumizi ya wanyama na binadamu, vinginevyo watapotea kama walivyopotea katika mabara mengine," anasisitiza.

### UWINDAJI WA SIMBA

Anasema simba ni miongoni mwa kundi la wanyama muhimu watano (big five) ambao watalii husafiri kuja kuwaona (simba, nyati, tembo, faru na chui).

"Kwenye utalii wa picha kuna wanyama mtalii akija ana hamu awaone na wakiwepo katika eneo linapandisha hadhi, na katika utalii wa uwindaji wanyama kama simba na chui mwindaji hupewa siku 21, kibali chake ni Dola 12,000 (zaidi ya Sh. milioni 28), ikiwa ni nje ya huduma nyingine kama malazi, waongoza watalii na magari," anafafanua.Kadhalika simba ni gharama kwa kuwa yupo katika orodha ya wanyama ambao hawaotikani kirahisi, mtalii anapotaka kuwinda nyumbu hupewa siku saba na ada si zaidi ya Dola 2,500 (zaidi ya Sh. milioni 5.7) na kwamba umuhimu na thamani ya simba ni kubwa.

### AINA ZA SIMBA

Simba wanaopatikana Tanzania ni aina moja, lakini kuna tofauti wa vinasaba kutokana na mazingira yao kama wa Selous na Serengeti au maeneo mengine, na kwamba simba wa Ngorongoro wana manyoya makubwa kwa sababu ya chakula wanachopata.

Februari mwaka huu, Mtafiti wa simba kutoka TAWIRI, Dk. Dennis Ikunda, alisema Tanzania ni kitovu cha simba duniani kwa kuwa kati ya asilimia 40 ya mnyama huyo duniani hupatikana nchini, na kati ya idadi hiyo wanapatikana katika ikolojia ya Serengeti mkoani Mara.

### BURUNGE WMA

Katibu wa Burunge WMA, Benson Mwaise, anasema changamoto kubwa iliyopo ni uharibifu wa mazingira ikiwamo kulipiza kisasi baada ya wanyama kula mifugo au kuharibu mazao, na kwamba wanatoa elimu kwa wananchi.

Pia, anasema faida ni kubwa kwa kuwa mwaka jana walipata zaidi ya Sh. bilioni mbili ambazo Sh. bilioni moja ziligawanywa katika vijiji 10 zilivyotoa eneo na kuunda WMA hiyo na kila kijiji kilipata Sh. milioni 103.

Naye Spika wa Burunge WMA, Marcel Yenoo, anasema ongezeko la mifugo ni kubwa ambalo limesababisha kuwa na mimea vamizi na kupungua eneo la malisho kwa wanyama pori na mifugo, jambo ambalo linahitaji ushirikiano wa pande zote kukabiliana na hali hiyo.

# Wazazi mbaroni madai ya kumuoza mwanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga lina washikilia watu wanne wakiwamo wazazi, kwa tuhuma za kumwozesha mwanafunzi wa darasa la tano (jina limehifadhiwa), mwenye umri wa miaka 12.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Debora Magiligimba, alitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari, na kubainisha kuwa ndoa ya mwanafunzi huyo iliyokuwa inafungwa saa 12 jioni waliitibua.

Alisema baada ya kupata taarifa za kufungwa kwa ndoa hiyo, walifika eneo la tukio wakiwa na maofisa Maendeleo ya Jamii wa halmashauri hiyo na kuwakamata watu wanne wakiwamo wazazi, huku bwana harusi akitoroka.

"Ndoa ya mwanafunzi huyu wa darasa la tano ilikuwa ina fungwa nyumbani kwao na bwana harusi Khalifani Japhari (23), baada ya kufika kwenye sherehe hiyo tuliwakamata watu wanne wakiwamo wazazi, kwa kosa la kumwozesha mwanafunzi na kumkatisha masomo," alisema Magiligimba. "Tulifanikiwa kuwakamata Geni Bundala, Jumanne Shigimahi, Hawa Ramadhani, na Japhari Khalfani, bwana harusi Khalfani Japhari, alitoroka na tunaendelea kumsaka ili wote wachukuliwe hatua kali za kisheria," aliongeza.

Kamanda alisema mwanafunzi huyo aliolewa kwa mahari ya ng'ombe wanane na Sh. 600,000. Vile vile, alisema mwanafunzi huyo wamempeleka kwenye kituo cha kulelea watoto waathirika wa mimba na ndoa za utotoni (Agape), kilichopo Manispaa ya Shinyanga. Alitoa wito kwa wazazi mkoani humo kuacha tabia ya kuozesha wanafunzi na kuzima ndoto zao.



Mgombea ubunge wa Ubungo kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Profesa Kitila Mkumbo, akilakiwa na vijana wanaofanya kazi kwenye gereji na bodaboda eneo la Manzese, Dar es Salaam jana, wakati wa kampeni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilo 103,953 za korosho kuteketezwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

JUMLA ya kilo 103,953 za korosho zilizokosa wanunuzi wilayani Kilwa, mkoani Lindi, zinatarajia kuteketezwa iwapo wamiliki hawataziondoa kwenye maghala ili kupisha nyingine.

Kiasi hicho cha korosho zinazoelezwa za daraja la tatu na kutokuwa na ubora unahitajika na wanunuzi, wakiwamo wabanguaji wadogo za msimu mwaka uliopita 2019.

Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Ubora wa Bodi ya Korosho, Domina Mkangala, aliyasema hayo wakati akijibu maswali ya wajumbe akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, wakati wa kikao cha tathmini ya ufuta, mbaazi na maandalizi ya msimu wa korosho kilichofanyika mjini Lindi. Ngubiagai alitaka kufahamu jitihada zinazochukuliwa kuziondoa kilo 103,953 za korosho zilizopo ghala la Nangurukuru, Wilaya ya Kilwa ili kupisha kuingizwa zingine za msimu wa mwaka huu.

Akijibu swali hilo na mengineyo kwa niaba ya Kaimu Mkurugenzi wa Bodi hiyo ya Korosho nchini, alisema kwamba korosho hizo zitateketezwa wakati wowote kuanzia sasa, iwapo wenye bidhaa hiyo hawatakuwa tayari kuziondoa wenyewe kutoka katika ghala hilo.

"Kimsingi siwezi kutamka hapa kuwa lini tutaziteketeza, lakini tunaomba kama wiki hivi, ili tukutane na wenye korosho, majibu watakayotupatia tutachukuwa hatua," alisema Mkangala.

Alisema kabla ya utekelezaji wake, uongozi wa bodi utalazimika kukutana na viongozi wa Chama Kikuu cha Lindi Mwambao pamoja na wakulima waliohusika kupeleka bidhaa hiyo ghala la Nangurukuru, ili kutoa nafasi ya kuingiza korosho zingine mpya msimu wa mwaka huu. Kaimu mkurugenzi huyo alisema iwapo korosho hizo zitarejeshwa kwa wakulima husika kuna hatari ya kuchafua soko na sifa ya nchi katika masuala ya kibiashara na mataifa mengine.

Alisema zoezi la uteketezaji wa korosho hizo kilo 103,953 litafanyika kwa kushirikisha Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC).

Kwa upande wake mwenyekiti wa kikao hicho ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alimwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo kusimamia zoezi hilo kwa ukaribu zaidi, ili kuziba mwanya kwa watakaohusika na zoezi hilo kuzitorosha.

# Sugu aibukia Songea kuwanadi wagombea

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya CHADEMA, Joseph Mbilinyi, ameibukia Songea Mjini kuwaombea kura mgomea urais wa chama hicho, ubunge katika jimbo hilo na diwani.

Aidha, amesema iwapo chama hicho kitaongoza nchi kitahakikisha kitaweka vizuri mifumo kwa wafanyabiashara na malipo ya stahiki za wafanyakazi ikiwamo kuongeza mishahara kwa wakati.

Mbilinyi maarufu kwa jina la Sugu aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa akiwaombea kura mgombea urais, Tundu Lisu, mgombea ubunge Jimbo la Songea Mjini, Adeni Mayalla na madiwani wa majimbo ya Songea Mjini, Peramiho, Madaba na Namtumbo kwenye viwanja vya mkutano Shule ya Msingi Matarawe, uliohudhuriwa na mamia ya wananchi.

Kwa mujibu wa Lissu, kwa miaka mitano vyama vya upinzani vilipigwa marufuku kufanya mkutano ili kuelezea sera za vyama vyao na kwa siku chache walizoruhusiwa wameona jinsi anakubalika na kuwataka wananchi kuhudhuria kwa wingi kila mkutano ili kusikia ilani na sera za CHADEMA ili wafanye maamuzi Oktoba 28, mwaka huu.

Mbilinyi alisema CHADEMA ndiyo chama pekee kilichobeba matarajio ya wananchi ambao wanahali mbaya ya kiuchumi na kwamba pia hali za watumishi wa serikali wakiwamo walimu wa shule za msingi, sekondari na vyuo ni ngumu kwa kuwa kwa muda wote hawajaongezewa mishahara.

"CHADEMA ikipata ridhaa ya kuongoza nchi itahakikisha kuwa wanaboresha uchumi kwa wananchi pamoja na kuongeza mishahara kwa watumishi wa serikali na taasisi binafsi," alisema.

Mgombea udiwani kwa tiketi ya CHADEMA kata ya Matarawe, Belokmansi Ponera, aliwaomba wananchi kuona umuhimu wa kumchagua kuahidi kushirikiana na serikali na wananchi kuimarisha miundombinu ya barabara, kujenga vyoo vya shule za msingi za Mwembe Chai, Sabasaba na Matarawe.

Aidha, alisema shule mbili za mwembe chai na Matarawe kwa muda mrefu zinatumia choo kimoja jambo ambalo alidai kuwa ni kero kubwa ambayo ataimaliza.

Naye Mwenyekiti wa CHADEMA mkoani Ruvuma, Christian Ruta, alisema chama hicho ni imara na kimejipanga kikamilifu kwa kuhakikisha kuwa kinafanya kampeni za kistaarabu na kuwaomba wananchi kutunza kadi zao za kupigia kura, ili Oktoba 28 waende kwenye vituo vyao vya kupigia kura na kuwachagua wagombea wa chama hicho.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kubanwa Simba, Yanga Bara, dalili soka linakua

**RAUNDI** ya tatu ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 inatarajia kukamilika leo kwa timu nne kushuka kwenye viwanja viwili tofauti hapa nchini.

Kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga Mwadui FC wataikaribisha KMC FC kutoka jijini, Dar es Salaam na Gwambina FC kutoka Mwanza wao watawafuata Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Mabatini, ulioko Mlandizi mkoani Pwani.

Tangu pazia la msimu mpya lilipofunguliwa Septemba 6, mwaka huu, timu zote zimeendelea kujipanga kwa lengo la kuwania pointi tatu muhimu kila wanaposhuka uwanjani na hali hiyo imezifanya mechi zote kuwa na ushindani.

Hadi kufikia jana, jioni (kabla ya mchezo kati ya Simba dhidi ya Biashara United kuchezwa), ni mechi moja tu ndio imeshuhudiwa kuwa na matokeo makubwa tofauti na ilivyokuwa inatarajiwa.

Mechi hiyo ni kati ya KMC dhidi ya Mbeya City, ambapo kikosi cha Manispaa ya Kinondoni kilipata ushindi mnono wa mabao 4-0.

Hata hivyo, matokeo ya baadhi ya mechi yamekuwa yakishangaza kwa dakika 90 kumalizika na matokeo kuwa tofauti na ilivyotegemewa, wakati 'watoto wa mjini' wakisema msije na matokeo mfukoni.

Ushindani unaoonyeshwa na timu zinazoitwa ndogo, unaonekana kuwasumbua vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga, ambao mashabiki na wanachama wao waliamini wangekuwa wanavuna idadi kubwa ya mabao baada ya kuamini usajili waliofanya.

Hali imekuwa tofauti, licha ya vigogo hao kutopoteza mchezo hata mmoja, lakini wamekuwa wakimaliza dakika 90 kwa jasho huku wakinusurika chupuchupu kufungwa na timu walizokutana nazo.

Nipashe inaamini ushindani huo na kitendo cha Simba na Yanga kubanwa ama nyumbani au ugenini, ni ishara nzuri kwa maendeleo ya mpira wa soka hapa nchini, kwa sababu ligi hiyo ndiyo inayotoa idadi kubwa ya wachezaji wanaounda kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).


Kufanya vizuri kwa timu hizo za mikoani, kunasaidia kuwaimarisha wachezaji na kuwaweka tayari kushindana katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ngazi ya klabu na kuelekea mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa upande wa Taifa Stars.

Ni wakati mwingine kwa wachezaji kuongeza bidii ili kutangaza vipaji vyao kwa mawakala mbalimbali ambao wanafuatilia kwa karibu mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo msimu huu zote zinaonyesha mubashara na kituo cha televisheni kilichopewa haki ya matangazo hayo.

Bado wachezaji hamjachelewa, ligi ndiyo imeanza, pambaneni na kwa kusaka matokeo chanya katika kila mechi na kuacha tabia ya kudharau baadhi ya michezo.

Pia nazikumbusha timu zilizoanza vyema msimu huu, kuendelea kujiimarisha katika mbio za ubingwa kwa sababu hakuna kisichowezekana, kama Leicester City iliweza kushinda taji la Ligi Kuu England msimu wa 2015/16 hata Ruvu Shooting inaweza kufanya hivyo kwa kulibeba taji hilo linaloshikiliwa na Simba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Viwanja vya Karume, Gwambina vilipitishwaje?

**BAADA** tu ya mechi za ufunguzi wa Ligi Kuu Bara, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TBLB), ilitangaza kuvifungia viwanja vya Karume mjini Musoma, Mara na wa Gwambina uliopo Misungwi jijini, Mwanza kutokana na kutokidhi baadhi ya vigezo.

Na hii ni baada ya watu wengi waliokuwa wakiangalia mechi hizo kwenye televisheni kushangaa na kutoridhishwa mwonekano wa viwanja hivyo.

Ukiangalia kwenye picha za televisheni, mechi zilizokuwa zinachezwa kwenye viwanja hivyo, hali ya uwanja pamoja na wachezaji jinsi walivyokuwa wakicheza, ilitengeneza mazingira fulani yanayochekesha, kushangaza na kusikitisha kwa wakati mmoja.

Uwanja wa Gwambina ndiyo ulioanza kufungiwa, mapema tu baada ya mechi kati ya Gwambina FC dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa Septemba 11, mwaka huu, mchezo uliomalizika kwa sare ya bila kufungana.

Mechi hiyo iliyoonyeshwa moja kwa moja kwenye televisheni, ilionekana kuwashangaza wengi na mitandao ya kijamii 'ikachafuka' kwa mshangao kutoka kwa mashabiki na picha mbalimbali.

Nadhani hii ndiyo moja kati ya sababu iliyoifanya Bodi ya Ligi 'kuutia kufuli' uwanja huo.

Taarifa ya haraka ya bodi hiyo ikatoka ya kuufungia Uwanja wa Gwambina kutokana na sehemu yake ya kuchezea kutokuwa na hali nzuri, kinyume na kanuni, na pia kuitaka klabu ya Gwambina kuchagua viwanja vya CCM Kirumba au Nyamagana kwa ajili ya kuchezea ligi.

Siku mbili baadaye wasimamizi hao wa soka nchini wakaufungia Uwanja wa Karume, lakini tayari timu ya Biashara ikiwa imeshacheza mechi mbili, dhidi ya Gwambia FC mechi ya ufunguzi na kushinda bao 1-0, lakini dhidi ya Mwadui, ikishinda pia bao 1-0.

Taarifa ya Bodi ya Ligi ilisema Uwanja wa Karume umefungiwa kwa sababu ya ubovu wa eneo la kuchezea, na vyumba vya kubadilishia nguo kutokidhi vigezo.

**Siku mbili baadaye wasimamizi hao wa soka nchini wakaufungia Uwanja wa Karume, lakini tayari timu ya Biashara ikiwa imeshacheza mechi mbili, dhidi ya Gwambia FC mechi ya ufunguzi na kushinda bao 1-0, lakini dhidi ya Mwadui, ikishinda pia bao 1-0.**

Ukiangalia hii pia ilitokana na mechi zote hizo mbili kuonekana kwenye televisheni na mashabiki wa soka kuanza kulalamika. Ingawa viwanja vingi vya mikoani si vizuri sana, lakini hivi vilivyofungiwa vilionekana vibovu zaidi.

Hapa najiuliza kama viwanja hivi visingeonekana kwenye televisheni vingefungiwa?

Nadhani uwezekano wa kuendelea kutumika ungekuwa mkubwa kwa sababu tayari vilikuwa vimeshaanza kutumika na kufungiwa ilitokana tu na watu wengi huhoji uhalali wa viwanja hivyo kupitishwa.

Kingine cha kujiuliza ni kwa nini Kamati ya Ukaguzi ilipitisha viwanja hivyo? Je, wakaguzi walikwenda kukagua kiwanja kwa kiwanja, au walipewa taarifa tu kuwa vipo sawa, ama walipelekewa picha ya viwanja kwa njia ya mtandao?

Pamoja na kuipongeza Bodi ya Ligi kufanya haraka kuamua jambo hili, lakini pia imetia doa kwa Kamati ya Ukaguzi wa viwanja na kuonekana haikufanya kazi yake sawasawa.

Inawezekana kamati ilikuwa inaamini Uwanja wa Gwambina uko vizuri kama ulivyokuwa ukionekana siku za mwanzo baada ya ujenzi, kwa hivyo walionekana kufanya kazi kimazoea.

Hapa kuna cha kujifunza kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi na Kamati zake kuwa zisifanye kazi kimazoea, badala yake zifanye kwa kufuata misingi, kwani kama kamati ile ingefanya ukaguzi wa kina, sidhani kama Gwambina na Biashara zingeanza kucheza mechi zao kwenye viwanja hivyo.

Na wengi wanajiuliza kama mechi zile zisingekuwa zinaonekana kwenye televisheni, basi mechi zingeendelea kuchezwa kwenye viwanja hivyo, labda pale tu siku Simba, Yanga na Azam zingekwenda kucheza ndipo kila mmoja wangeshtuka, lakini wakati huo baadhi ya timu tayari zimeshaumia kucheza kwenye viwanja vibovu.

## HABARI KITAIFA

# Tunduma kubadilishwa kitovu cha uwekezaji, biashara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeweka mkakati wa kuubadilisha mji wa Tunduma, Mkoa wa Songwe kuwa kitovu cha biashara ya kikanda kwa nchi za Afrika na bara la Asia, utakaozalisha ajira na kukuza eneo hilo mpakani kuwa moja ya majiji makubwa nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Profesa Riziki Shemdoe, alisema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati akiongea na viongozi wa serikali kutoka Mkoa wa Songwe waliokuwa katika ziara ya mafunzo eneo la Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA).

"Mji wa Tunduma uko katikati ya masoko ya kikanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, unaweza kuunganisha soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na mengine. Ni wakati muafaka wa kutekeleza mpango huu ambao utanufaisha Watanzania kupitia fursa zitakazoibuliwa na mkakati huu," alisema.

Mkurugenzi wa Uwezeshaji Uwekezaji wa EPZA, James Maziku, alisema kuwa mji wa Tunduma si lango la nchi za SADC pekee, bali sehemu kubwa ya bara la Afrika kwa kuwa biashara zaidi ya ulimwengu inafanyika katika nchi za Asia, ambayo inafanya Bahari ya Hindi kuwa ukanda wa biashara.

"Kampuni za kimataifa zinaweza kuvutiwa kuwekeza katika eneo la Tunduma kwa kuwa itakuwa rahisi kusafirisha bidhaa kutoka mji wa Kampiri Mposh, Zambia na kuziuza kwa soko la Asia kwa urahisi zaidi.

Mkoa wa Songwe pia una utajiri wa ardhi yenye rutuba inayofaa kwa kilimo na mkoa huo unashika nafasi ya tatu katika uzalishaji wa mazao mbalimbali kwenye mikoa 26, alisema Dk. Shekalaghe. Rasilimali nyingine ni pamoja na madini ya dhahabu, shaba na chumvi na utalii.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe (RAS) Dk. Seif Shekhalage, alimwambia Katibu Mkuu huyo kwamba mkoa wake umetenga eneo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 400 kwa ajili ya kujenga ukanda maalum wa kiuchumi (special economic zone-SEZ), ambao utavutia ujenzi wa miradi ya kimkakati ya maendeleo ya kiuchumi.

"Eneo lililotengwa kwa ajili ya SEZ litavutia wawekezaji wa kujenga viwanda na bandari kavu kutokana na takwimu kuonyesha karibu asilimia 70 ya shehena iliyoingizwa kupitia bandari ya Dar es Salaam kuelekea nchi za SADC hupitia mpaka wa Tunduma," alisema.

Pia, alisema eneo la Tunduma litaweza kuwa kivutio cha viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la nchi za SADC wakati bandari kavu pendekezwa itapokea shehena kutoka Dar es Salaam kupitia reli ya Tanzania-Zambia Railways (TAZARA), inayopita karibu na mji wa Tunduma kabla ya kusafirishwa kwenda nchi za nje.

"Hii itakuza biashara zaidi na kutoa ajira kwa kuwa hivi sasa, jumla ya malori ya mafuta 120 na malori 80 ya mizigo mingine na magari mapya (IT) 120 hupita katika mpaka wa Tunduma kuelekea nchi za Zambia, Malawi, Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kila siku," alisema.




Meneja Uhusiano Serikalini wa Benki ya NBC, William Kallaghe (kushoto), akielezea kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo, mahususi kwa ajili ya wadau wa sekta ya madini nchini kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (katikati), pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel (kulia), wakati viongozi hao walipotembelea banda la benki hiyo kwenye viwanja vya maonyesho ya dhahabu na teknolojia vya Bombambili mkoani Geita. **MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo, wajasiriamali waonyeshwa fursa taasisi za fedha

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAKUU wa mikoa ya Mwanza na Geita wamewaomba wachimbaji wadogo na wajasiriamali katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kuhakikisha wanatumia ipasavyo ushiriki wa taasisi za fedha kwenye maonyesho ya dhahabu na teknolojia yanayoendelea.

Wametakiwa kuyatumia maonyesho hayo mkoani Geita ili kujijengea uelewa wa kutosha katika masuala ya kifedha na mitaji.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel walitoa wito huo mwishoni mwa wiki walipotembelea mabanda ya washiriki pamoja na kuzungumza na wananchi waliotembelea maonyesho hayo ya siku kumi kwenye viwanja vya Bombambili.

"Kupitia maonyesho haya habari njema imekuwa ni ushiriki mzuri wa taasisi za fedha ikiwamo Benki ya NBC ambao pamoja na kudhamini maonyesho haya, pia wanaendesha mafunzo kwa wajasiriamali na wachimbaji wadogo. Hii ni hatua kubwa, na wito wangu kwa washiriki ni kuhakikisha wanatumia vema fursa hii kujijengea uwezo wa kuendesha shughuli zao kwa ufanisi na kwa viwango bora," alisema Mongella.

Mongella aliongeza kuwa kupitia maonyesho hayo, taasisi mbalimbali za kifedha zimeweza kutangaza huduma mbalimbali ikiwamo mikopo mahsusi kwa ajili ya wadau wa madini wakiwamo wachimbaji wakubwa na wadogo pamoja na wajasiriamali, huku akitolea mfano mafunzo yanayotolewa na Benki ya NBC na wadau wengine kuwa yatawasaidia kujenga uelewa wa kutosha wadau hao hususani katika masuala ya kifedha na uendeshaji wa shughuli za madini kisasa.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Gabriel, alisema kupitia maonyesho hayo, mkoa huo unatarajia mapinduzi makubwa ya kiuchumi kutokana na mageuzi makubwa ya uendeshaji wa shughuli za kiuchimbaji na biashara yanayotarajiwa kufuatia mafunzo yanayoendelea kufanywa na taasisi mbalimbali kwa wachimbaji wadogo na wajasiriamali. "Ndio maana tunashukuru sana taasisi za fedha hususani benki ya NBC ambayo ndio wadhamini wakuu kwenye mafunzo haya kwa kuwa chachu ya mabadiliko tunayoyatarajia. Pia, ushiriki wa taasisi nyingine kwenye mafunzo haya ikiwamo TANTRADE, Tume ya Madini, TRA, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, NSSF, GST, SIDO, NEMC, TBS, OSHA na NEEC unatuhakikishia mabadiliko tunayoyatarajia," alisema Mhandi Gabriel.

Akifafanua kuhusu huduma na ushiriki wa benki hiyo kwenye maonyesho hayo, Mkuu wa Kitengo Cha Mahusiano na Serikali Benki ya NBC, William Kallaghe, alisema mbali na mafunzo hayo, benki hiyo inaendesha kliniki ya biashara kwa ajili ya wajasiriamali ili waweze kunufaika na mnyororo wa biashara ya madini.

"Ni wingi wa huduma maalumu kwa wadau mbalimbali ndio unaosababisha benki ya NBC tuweze kushiriki kwenye maonyesho ya wadau tofauti tofauti yakiwamo maonyesho haya ya dhahabu na teknolojia," alibainisha Kallaghe.

# Wanaohitimu elimu ya juu waaswa kung'ang'ania Dar es Salaam

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka vijana wanaohitimu elimu ya juu kuacha kuchagua maeneo ya kufanya kazi wanapopangiwa ajira mpya, kwani maeneo ya vijijini kuna watu wanaohitaji huduma pia.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Selemani Jafo, wakati wa mahafali ya pili ya wanafunzi waliosoma nje ya nchi, yaliyoandaliwa na Global Education Link (GEL).

Waziri alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya vijana kupenda kufanya kazi jijini Dar es Salaam na kuacha kwenda kwenye maeneo ya vijijini wanayopangiwa wanapoajiriwa.

"Serikali itakapoajiri itawapa kipaumbele vijana mliohitimu kupitia Global, lakini lazima mtambue kuwa vijijini kuna Watanzania ambao wanahitaji huduma zenu pia, mkipangiwa nendeni popote pale mking'ang'ania Dar es Salaam nawahakikishia mtakwama," alisema Waziri Jafo.

Waziri Jafo aliipongeza GEL kwa namna ambavyo imekuwa ikifuatilia maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi hao kuhakikisha wanahitimu tena kwa viwango vinavyokubalika kimataifa.

"Kama kuna Watanzania wazalendo basi wewe Abdulmalik Mollel ni mzalendo sana, wewe na timu yako mnafanya kazi kubwa na nzuri sana mnalisaidia taifa hili kusonga mbele kwa sababu vyuo tulivyonavyo na fani hatutoshelezi inabidi twende kusoma na nje pia mmeweka utaratibu mzuri," alisema Jafo.

Waziri alimshauri Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik kuanzisha siku maalum ya GEL ambapo atakuwa akiueleza umma kuhusu fursa za wataalamu waliopo na wanaotarajiwa kupatikana kupitia taasisi hiyo.

Aidha, Waziri Jafo alisema serikali inaunga mkono shughuli zote zinazofanywa na GEL na itaendelea kushirikiana nayo kwani imeonyesha uzalendo wa hali ya juu katika kuisaidia Tanzania kupata wataalamu.

Kwa upande wake, Abdulmalik aliishukuru serikali kwa ushirikiano inaompa katika kutekeleza majukumu yake na aliahidi kuwa ataendelea kufuatilia mwenendo wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje.

Alisema mbali na kuwapeleka litakuwa jukumu lake kuhakikisha wanaporudi nyumbani wanaunganishwa na waajiri ili ujuzi walioupata uwe na manufaa kwa nchi yao.

# Zaidi ya wanyamapori 300 hufa kwa kugongwa na magari

**Na Salome Kitomari**

WANYAMAPORI 380 wamekufa kwa kugongwa na magari katika mapito ya wanyama ya Kwakuchinja, yanayopitiwa na barabara kuu ya Arusha-Babati.

Mtafiti wa simba wa ikolojia ya Manyara Tarangire, Dk. Bernard Kissui, aliwaambia waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), waliofanya ziara ya kutembelea eneo hilo kwa lengo la kuandika habari za uhifadhi, ujangili na changamoto zilizopo.

Ziara hiyo iliwezeshwa na Shirika la Misaada la Marekani kupitia mradi wa Protect (USAID Protect).

Alisema walibaini kuwa kila siku mnyama mmoja anagongwa na gari na katika uchambuzi wao walibaini aina tofauti 50 hugongwa na magari na wengi ni wanyama wanaozaa (Mamalia) na wanaotaga.

"Barabara ni nzuri, lakini kwenye maeneo ya hifadhi lazima tufanye kitu, kama tunahifadhi ni lazima tujue la kufanya ili kuwalinda wanyama na shughuli kuendelea," alisema.

Alisema walianza ufuatiliaji kuanzia eneo la Magugu hadi Makuyuni, umbali wa kilomita 58, na kila siku kuna vijana wanatembea na pikipiki asubuhi na jioni kupiga picha na kurekodi wanyama aliouawa kwa kugongwa, ili kuonyesha madhara ya barabara.

Alisema wapo wanaogongwa ambao wanapendwa na binadamu na huwachukua kabla ya kurekodiwa na kwamba idadi inaweza kuwa kubwa kwa kuwa kuna eneo la Makuyuni hadi Mtoambu ambako kote wanyama hupita kwenda maeneo mengine yaliyohifadhiwa.

Alisema maeneo ya shoroba ya Kwakuchinja ambayo tembo hupita kwa wingi ndiyo kuna wanyama wengi wanaouawa, jambo ambalo linaonyesha kuwa ni lazima hatua zichukuliwe kuokoa.

"Tunaendelea kukusanya takwimu na hadi sasa wanyama wanaendelea kuuawa, tunaonyesha hali halisi ikiwa ni mfano wa eneo moja kati ya mengi yaliyopitiwa na barabara kuu, tunaona wanyama wanateketea," alisema.

"Tumetoa mapendekezo ambayo yamefanyika kwingine kama kujenga barabara za juu na wanyama wapite chini au wanyama wapite juu na barabara chini, vinginevyo idadi itaendelea kupungua na itaathiri utalii," alisema.

Dk. Kissui alisema shoroba zinazidi kupungua na utafiti umeonyesha kuwa mwaka 1964 zilikuwa zaidi ya 10, mwaka 1985 zilibaki tano, mwaka 2011 zilibaki tatu na sasa imebaki moja.

Alisema ikolojia ya Manyara Tarangire ni muhimu kwa uchumi wa nchi, utalii na maendeleo ya jamii, na kwamba Hifadhi ya Jamii (Burunge Wildlife Management Area (WMA), ni muhimu kwa ukuaji wa eneo hilo.

"Utalii wetu Tanzania na mafanikio yake makubwa yanayotokana na kuwapo kwa wanyama yanategemea sana mifumo ya kiikolojia inavyoweza kufanyakazi kwa pamoja, ndiyo maana Burunge WMA ni muhimu sana katika ikolojia ya Tarangire na Manyara," alibainisha. Eneo la ikolojia ya Manyara Tarangire lina ukubwa wa kilomita za mraba 35,000, linahusisha hifadhi za taifa za Manyara na Tarangire, maeneo yaliyohifadhiwa ya Mkurunero, Hifadhi za jamii za Burunge, Randlen, Makame, Ziwa Natron pamoja na maeneo ya hifadhi ya Mtoambu, Lokusare, Kitwai na Simanjiro lenye ukubwa wa kilomita za mraba 35,000.




Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni Dar es Salaam, Rose Mgeta (katikati), jana, akiongoza wachungaji na waumini wengine katika maombi ya kuliombea amani taifa kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usajili wa viwanda vidogo vya usindikaji mazao kurahisishwa

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, amesema serikali inaangalia uwezekano wa kupunguza mlolongo wa mchakato wa uanzishaji viwanda vidogo vidogo hasa vya usindikaji wa mazao ya chakula ili kupunguza upotevu wa mazao wakati wa mavuno.

Alisema hayo wakati wa kongamano la kitaifa la wadau wa jukwaa la kuzuia upotevu wa mazao wakati wa mavuno, ambapo inakadiriwa zaidi asilimia 30 ya mazao hayo hupotea, hivyo kutishia kupungua kwa ziada ya chakula kwa baadhi ya mikoa.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikiwaathiri wakulima wengi, serikali itapitia upya mfumo wa usajili ili wawekezaji wajitokeze kwa kuanzisha viwanda vingi vya usindikaji wa mazao ya chakula.

"Kuna mlolongo mrefu pale Mtanzania au mwekezaji anapotaka kuanzisha kiwanda kidogo, wakati mwingine inawakatisha tamaa kwa hiyo kama serikali tutakaa na wadau wengine kuangalia jinsi ya kupunguza mchakato wa uanzishaji viwanda vya uchakataji mazao, ili kupunguza upotevu wa mazao wakati wa mavuno," alisema Kusaya.

Audax Lukonge, Mkurugenzi wa Taasisi ya ANSAF, alisema kuwa pamoja na kwamba lengo la kupunguza upotevu wa chakula ni kufikia asilimia 50 kufikia mwaka 2025, lakini ipo haja ya nchi kuona umuhimu wa kuongeza jitihada katika kuzuia upotevu huo.

Alisema endapo jitihada za makusudi zitachukuliwa kwa kushirikiana kati ya serikali na wadau wengine, upo uwezekano wa kupunguza changamoto ya upotevu wa mazazo hadi kufikia asilimia 75 ukizingatia Tanzania imefanikiwa kuingia katika uchumi wa kati katika kipindi kifupi.

"Kama Tanzania tumeweza kufikia uchumi wa kati katika kipindi kifupi cha miaka mitano, basi tunaweza kushirikiana na wadau wote ili changamoto tukaipunguza kwa asilimia 75 mpaka kufikia 2025," alisema Lukonge.

## Morogoro yajikita kilimo cha korosho

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imeanza mkakati wa kulifufua zao la korosho katika Mkoa wa Morogoro, ili kulifanya zao hilo kuwa moja ya mazao ya biashara litakalosaidia kukuza uchumi wa mkoa huo.

Kupitia mkakati huo, TARI Naliendelea iliyopo mkoani Mtwara imeanza kutoa mafunzo kwa wakulima wa korosho kwa mkoa wa Morogoro, ili kuwapatia mbinu bora za uzalishaji wake.

Akizungumza katika mafunzo hayo yaliyohusisha wakulima wa zao hilo na maofisa ugani, Mratibu wa zao la korosho kutoka TARI, Dk. Geradina Mzena, alisema lengo ni kutaka kumwondoa mkulima kutoka katika kilimo cha kujikimu na kuanza kulima kilimo cha biashara.

Alisema kwa kuwa Morogoro kuna wakulima wapya, lengo ni kukifanya kilimo cha korosho kuwa cha kibiashara, hivyo ni lazima kuwapatia mafunzo ya namna ya kutunza zao hilo na changamoto mbalimbali za kilimo hicho.

"Tunatambua hii ni mikoa mipya yenye wakulima wa zao la korosho, hivyo tumeona kuwa tuwapatia mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho, ili waweze kulima kilimo cha kibiashara," alisema Dk. Mzena.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Neema Marwa kutoka wilayani Mvomero, alisema ameamua kuanza kulima korosho, baada ya kuhamasika na kuwa na uhakika wa soko lake ukilinganisha na kilimo cha mazao mengine ya biashara.

Naye Martini Joseph, mkazi wa Morogoro Vijijini, aliishukuru serikali kwa kuamua kutoa mafunzo ya kilimo hicho ambacho kimekuwa na gharama nafuu na chenye kuleta tija na mafanikio kwa haraka tofauti na kilimo kingine.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji), Rosaria Rwegesira, alisema kwa miaka ya nyuma mkoa wa Morogoro ilikuwa miongoni mwa mikoa inayolima zao hilo, lakini kutokana na kutokuwa na soko la uhakika, wakulima walikata tamaa.

Alisema kutokana na hamasa katika miaka ya hivi karibuni, wakulima wameamua kuanzisha kilimo hicho ambapo mwaka 2018 zilipatikana jumla ya tani 63 na mwaka 2019 ziliongezeka kufikia tani 183, hivyo kupitia mafunzo hayo uzalishaji huo utaendelea kuongezeka na kuwa miongoni mwa mikoa ambayo inazalisha korosho.

HABARI KITAIFA

# CCM Dar yaja na kampeni kwa daladala

Na Elizabeth Zaya

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dar es Salaam, kimeanzisha mpango wa kufanya kampeni kwa kutumia basi maalum maarufu kama 'The CCM Campaign Bus' ambalo litakuwa likipita katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Kwa mujibu wa mratibu wa mpango huo, Jordan Balindo, basi hilo litakuwa linachukua watu kuanzia asubuhi mpaka jioni katika vituo vya daladala na kutakuwa na mijadala maalum ambayo itakuwa inajadiliwa na abiria wanaokuwa katika gari hilo. "Katika kutimiza mpango wa kufanya kampeni za kistaarabu, CCM wamekuja na mpango wa kufanya kampeni kwa njia ya basi dogo aina ya coaster lililopambwa kwa rangi za chama na picha za wagombea, likibeba watu kutoka kituo kimoja kwenda kingine ndani ya jiji la Dar Es Salaam, wakielekea katika shughuli zao za kila siku," alisema Balindo.

"Wakiwa ndani ya basi, abiria watasikiliza jumbe tofauti ikiwamo ya kutoa elimu namna ya kushiriki katika uchaguzi na kupiga kura kwa wale wenye sifa ya kufanya hivyo."

Balindo alisema lengo ni kufanya kampeni jumuishi kwa mwananchi wa aina yeyote.

"Katika mijadala itakayokuwa inaendeshwa katika basi letu, pia kutakuwa na kuuliza maswali, kutoa maoni, mitazamo kuhusu kazi na miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali ya CCM, na yatajibiwa na maofisa wabobezi wa chama na maoni yatachukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi," alisema Balindo.

"Tutajadili pia aina ya viongozi tunaowataka kuanzia rais, wabunge, madiwani, na tunataka watu wengi zaidi wafikiwe."

Alisema kampeni kupitia basi hilo hazitakuwa za kumzungumzia mtu wala kutoa maneno ya kashfa, bali zitazingatia katika kujadili hoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wao, faida za kushiriki katika uchaguzi hususani katika kupiga kura.

"Hatuko tayari kuwakaribisha watu wenye lugha za kuudhi na zenye kuleta tahaluki katika nchi yetu, tunahitaji watu wazingatie katika kujadili hoja tu na si vinginevyo," alisema Balindo.

Alisema kwa sasa mpango huo utajikita katika Jiji la Dar es Salaam na kwamba endapo itaonekana kuna umuhimu wa kuufikisha katika mikoa mingine watafanya hivyo.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla (wa pili kushoto), Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega (kulia), Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya NCBA Tanzania, Margaret Karume na kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara na Huduma za Kidigitali wa benki hiyo, Gift Shoko, wakionyesha chapa ya benki mpya ya NCBA Tanzania katika hafla ya uzinduzi wa matawi mapya mawili, mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA kudhibiti kero mitandaoni

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema itahakikisha inaendelea kudhibiti matatizo mbalimbali yatokanayo na mitandao ya mawasiliano, ili kukabiliana na wimbi la wizi mitandaoni.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Masoko wa TCRA Ofisi ya Zanzibar, Sofia Mabada, alipokuwa akitoa elimu kwa wadau wa TCRA katika mkutano uliofanyika ukumbi wa Maktaba Chakechake Pemba.

Alisema mamlaka hiyo itaendelea na mkakati wa kutoa elimu kwa wadau wake jinsi ya mtandao unavokua siku hadi siku, kwa lengo la kuona sekta hiyo inakuwa na mazingira salama kwa kila mdau.

Alieleza kuwa TCRA inasimamia suala zima la mawasiliano kwa maslahi mbalimbali ya serikali pamoja na wananchi wakiwamo watoaji na wapokeaji huduma kwa lengo la kupata huduma bora kwa wateja.

Alisema kukua kwa kasi sekta ya mawasiliano nchini na duniani kumechangia na ongezeko la huduma kwa watumiaji pamoja na watoa huduma hiyo.

Alisema mabadiliko katika sekta ya mawasiliano imeweza kuleta maendeleo makubwa na kurahisisha mambo mengi katika shughuli za kila siku, hivyo ni vyema kuutumia kihalali ili kila mmoja aweze kufaidika nao na sio kupata matatizo.

Issa Mohamed Salum kutoka makao makuu ya Polisi Zanzibar, alisema suala la kuzuwia uhalifu mitandaoni si jukumu la jeshi hilo pekee bali ni la watu wote hivyo ni vyema kutoa ushirikiano pale linapotokea tatizo hilo.

Abdalla Mbarouk kutoka TTCL Pemba, alisema kutokana na umuhimu wa wateja, ni vyema kutoa huduma iliyotukuka ili kila mmoja aweze kufaidika.

Mkutano huo uliowashirikisha wadau wa TCRA na kutoa elimu kusikiliza kero za wateja, maoni ya wateja na uzoefu uliopatikana.

# Wakulima wa kahawa Ngara wapata fursa zaidi

Na Mwandishi Wetu, NGARA

WAKULIMA wa kahawa wilayani Ngara mkoani Kagera wamepata fursa zaidi, baada ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Chama cha Kikuu cha Ushirika cha Ngara [NFCS-LTD) kukubaliana kuendelea kushirikiana ili kuinua uzalishaji wa kahawa na kukuza pato la wakulima wa zao hilo katika wilaya hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na kumnukuu Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, imesema kwamba baada ya mazungumzo kati ya viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika na TADB, pande mbili zimetambua haja ya kuendeleza ushirikiano kwa nia ya kuinua uzalishaji wa kahawa na kuinua pato la wakulima wadogo wa kahawa.

Taarifa ilisema kwamba viongozi wa chama hicho wamekieleza kikao cha pamoja kwamba changamoto wanazokumbana nazo watendaji wa ushirika ni pamoja na kutokuwa na vyombo vya usafiri na kwa hiyo wanashindwa kuwafikia wakulima kwa urahisi.

Aidha, wakulima hawana elimu ya kutosha juu ya uzalishaji wa kahawa na kwa hiyo kahawa inayozalishwa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya soko.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, benki imeahidi kutoa pikipiki mbili kwa viongozi wa ushirika ili waweze kuwafikia wakulima, imesema taarifa hiyo na kuongeza kwamba TADB iko tayari kutuma Ngara wataalamu ili watoe elimu ya uoteshaji wa miche ya mibuni mipya ikiwa ni mbinu mathubuti ya kuinua uzalishaji wa zao la kahawa. Chama hicho cha ushirika kilianzishwa 1993.

Hata hivyo kilisitisha huduma zake kwa wakulima mwaka 2012 kutokana na changamoto kadhaa ikiwamo ukosefu wa fedha ya kugharamia shughuli za chama na madeni ya kupindukia.

Mwaka 2018 TADB iliingilia kati na kukifufua chama hicho kwa kukitengenezea mfumo mzuri wa uendeshaji.

"Chama kilipewa mkopo wenye riba nafuu uliokipa uwezo wa kukusanya kahawa hadi kufikia tani 2,300 kutoka kwa wakulima wadogo zaidi ya 500 wilayani Ngara," taarifa hiyo ilieleza.

# Ushahidi wafuta kesi ya tuhuma za kubaka

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa wa Wete imeiondoa kesi namba 75 ya mwaka 2019 iliyokuwa inamkabili Khamis Abdalla Khamis (35), aliyetuhumiwa kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka kumi baada ya mashahidi kutofika mahakamani.

Akitoa uamuzi huo Mrajisi wa Mahakama Kuu Pemba, Abdul-razak Abdul-kadir Ali, alisema, analiondoa shauri hilo chini ya kifungu cha 103 (9) cha sheria namba 7 ya mwaka 2018.

"Kifungu hiki kinanipa uwezo wa kuliondoa shauri ikiwa mashahidi wameshindwa kufika mahakamani," alisema Mrajis huyo.

Alisema upande wa mashtaka unaweza kulifungua tena shauri hilo iwapo watawapata mashahidi na kuwapeleka mahakamani.

"Upande wa mashtaka mtakapopata mashahidi wa kesi hii basi mnaweza kulirudisha tena, lakini kwa leo nimeliondosha," alifafanua.

Kesi hiyo ilianzwa kusikilizwa kwa mara ya kwanza Oktoba 1, mwaka jana katika Mahakama ya Mkoa Wete.

Ilidaiwa na mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Juma Mussa Omar, kuwa mtuhumiwa anatuhumiwa kutenda makosa mawili.

Kosa anadaiwa alilitenda kati ya Septemba 01 na 20, mwaka jana saa zisizofahamika katika maeneo ya Konde Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo alimbaka mtoto mwenye umri wa miaka kumi.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume cha kifungu cha 108 (1) (2) (e) na 109 (1) cha Sheria ya adhabu namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

Kosa la pili alidaiwa kulitenda siku hiyo hiyo mwaka jana saa zisizofahamika Konde alimwingilia kinyume cha maumbile mtoto huyo.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume cha kifungu cha 115 cha sheria namba 6 ya mwaka 2018.




Mkazi wa Kigamboni jijini Dar es Salaam, Sada Bwamkuu, ambaye ni muwekezaji katika Kampuni ya Mr. Kuku Farmers Limited, akizungumza huku akilia mbele ya wawekezaji wenzake baada ya akaunti ya kampuni hiyo kufungiwa alizungumza hayo kwenye mkutano na vyombo vya habari uliofanyika Kigamboni jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIDO yahamasisha ujenzi wa viwanda

Na Enock Charles

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), limesema linajivunia kuwa sehemu ya mafanikio ya Tanzania kuingia katika orodha ya nchini ya uchumi wa kati sambamba na kufanikisha azma ya serikali ya kuwa nchi ya viwanda ifikipo mwaka 2025.

Aidha, SIDO imewaomba Watanzania kujenga viwanda ili kuboresha maisha ya watu kila pembe ya Tanzania kwa sababu umeme upo na unaendelea kufuliwa hadi kufikia MW 3,000 katika miaka mitatu ijayo.

Shirika limesema viwanda vitaibua maisha bora kila vitakapojengwa, hasa viwanda hivyo vitakuwa ni vya kuchakata mazao ya wananchi na vya kutengeneza vifaa vya kubadilisha maisha ya wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof. Sylvester Mpanduji, aliwataka Watanzania kuibua mawazo ya viwanda na kuyapeleka mawazo hayo katika ofisi za SIDO wilayani na mikoani ili yachambuliwe na kuanzisha viwanda na kuongeza kwamba SIDO ina matawi kila mkoa nchi nzima na ina wataalumu wa kutoa mafunzo ya kufanya biashara na kutumia teknolojia ili Watanzania wajiajiri katika nyanja mbalimbali ya ujasiriamali. Aliwaomba Watanzania kulitumia shirika hilo kujipatia elimu na mafunzo ya kuwawezesha kuanzisha viwanda vidogo kuchakata mazao yao na kuyaongeza thamani. "Tayari SIDO imeshajenga viwanda darasa katika maeneo mbalimbali nchini, lengo likiwa kuwawezesha wajasiriamali kupata mafunzo ya kuzalisha bidhaa zao katika mazingira wezeshi na kupatiwa vibali vyote vya mamlaka za nchi ili wafanye biashara ya uhakika," alisema Prof. Mpanduji.

Alitaja mikoa yenye viwanda darasa kuwa ni Dodoma, Mwanza, Simiyu, Kagera, Geita, Mtwara na Katavi. Kwa msukumo wa serikali ya Rais John Maguli na ushirikiano wa wadau wengine, SIDO imesimamia kwa mafanikio ujenzi wa viwanda 8,477 ambavyo vimezalisha ajira zaidi ya 500,000.

Kati ya hivyo viwanda 201 ni viwanda vikubwa, viwanda 460 ni viwanda vya kati, na 3,406 ni viwanda vidogo huku 4,410 ni viwanda vidogo kabisa.

Profesa Mpanduji amesema SIDO itaendelea kuimarisha idara ya teknolojia na ubunifu ili kuinua maendeleo katika sekta ya viwanda, na kutoa wito kwa Watanzania kutumia fursa ya uwepo wa SIDO kupata mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kujiajiri.

# Wasio na uwezo darasani kusaidiwa

Na Yamine Protace

SHULE ya Sekondari ya St Mark's iliyopo Kongowe Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam, imeandaa mkakati wa kuwatambua wanafunzi walio chini kiuwezo na kuwasaidia ili nao waweze kufanya vizuri kitaaluma.

Hayo yalisemwa na mwalimu mkuu wa shule hiyo, Leticia Kaijage, katika mahafali ya 17 ya shule hiyo.

"Tunatambua baadhi ya wanafunzi wanakuwa chini darasani, baada ya kubaini hilo shule imeandaa mkakati ambapo wanafunzi wasio na uwezo wanatambuliwa na kusaidiwa ili waweze kuinuka kielimu," alisema.

Alisema shule yao imekuwa na mafanikio makubwa katika ufaulu na hali hiyo kuifanya kuwa na matokeo mazuri kila mwaka, ambapo kidato cha nne katika mitihani ya mwisho wanafaulu na kujiunga na kidato cha tano na wengine kujiunga vyuo.

Aliongeza kuwa mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano uliopo mzuri baina ya walimu na wanafunzi katika masomo yanayotolewa.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana wanafunzi wa kidato cha nne walifaulu kwa asilimia 100, huku mwaka huo kidato cha pili walifaulu kwa asilimia 99.

Alisema, mafanikio hayo yamechangiwa na kuwa na walimu wa kutosha, maabara zenye vifaa vya kutosha na maktaba yenye vifaa vya kujifunzia.

Alisema shule yao imeanzisha klabu za wanafunzi kujisomea na hatua hiyo inasaidia ongezeko la ufaulu.

Aliwataka wahitimu wayaendeleze maadili na malezi bora waliyoyapa kipindi walichokuwa shuleni hapo.

# Vijana waonyeshwa fursa mpya ya ajira

Na Richard Makore, MWANZA

WAKAZI wa Jiji la Mwanza wakiwamo vijana wametakiwa kuchangamkia fursa za uzoaji wa takataka katika maeneo mbalimbali ili kujitengeneza ajira, hivyo kujiongezea kipato.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Afya katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Desderius Polle kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Philis Nyimbi, katika maadhimisho ya Siku ya Usafi Duniani yaliyofanyika eneo la Igogo.

Alisema eneo la uzoaji takataka lina fursa nyingi kama likitumiwa vizuri na wadau, kwamba linaweza kutoa ajira huku likisaidia kuliweka jiji katika hali ya usafi.

Aliitaka jamii kuunda vikundi na kuanza kujihusisha na uzoaji takataka katika maeneo mbalimbali wanayoishi jijini Mwanza.

Ofisa Mazingira wa Jiji la Mwanza, Fanuel Kasenene, alisema, Jiji la Mwanza lina magari 14 ya kuzoa takataka.

Aidha, alisema wametoa zabuni kwa kampuni nne ambazo kila siku zinafanya kazi ya kuzoa takataka na kuzipeleka dampo eneo la Buhongwanje kidogo ya jiji.

NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 21, 2020

Nipashe

Spotika



VIUNGO 10 BORA ZAIDI KARNE YA 21 UK. 12&13





# NYOTA WA5 WANAOTARAJIWA MAKUBWA EPL MSIMU HUU

PEPE

## ISIKUPITE

GARETH Bale ambaye wiki iliyopita alirejea Tottenham, aliifungia Real Madrid mabao 105 katika mechi 251 za mashindano mbalimbali aliyocheza. Kabla ya kuhamia Madrid, winga huyo wa Timu ya Taifa ya Wales aliifungia Spurs mabao 42 katika mechi 150 za Ligi Kuu England.




**LONDON,** England

ORODHA hii ni ya wachezaji watano ambao wanatarajiwa kufanya makubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England msimu huu wa 2020/21.

Orodha hii inawajumuishwa wachezaji wawili kutoka Manchester United na mmoja mmoja kutoka Manchester City, Arsenal na Chelsea.

**5- ANTHONY MARTIAL (Manchester United)**

Inaonyesha, Anthony Martial kama amesubiriwa kwa muda mrefu. Kwa misimu mingi, raia huyo wa Ufaransa hakuwa kwenye kiwango cha kuvutia.

Msimu uliopita ukaonekana kama ni bora zaidi kwa Martial na mashabiki wakaanza kuona kile walichokisubiri kwa muda mrefu. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, alifunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho saba katika mechi 32 za Ligi Kuu England msimu uliopita.

Msimu huu mashabiki wa Manchester United watatarajia mengi zaidi kutoka kwa Mfaransa huyo.

Huku dili la usajili wa Jadon Sancho likionekana kutofanikiwa pale Manchester United, Martial atakuwa na nafasi kubwa msimu huu.

**4- PHIL FODEN (Manchester City)**

Pep Guardiola aliwahi kumwelezea, Phil Foden kama mmoja wa wachezaji wenye vipaji vikubwa zaidi aliowahi kuwashuhudia. Hiyo ni kauli ya heshima kubwa kutoka kwa mtu aliyefanya kazi na Lionel Messi.

Foden anatajwa kama ndio mrithi wa David Silva kwenye kikosi hicho, hivyo maana yake msimu huu anaweza kupata mechi nyingi zaidi za kucheza.

**3- MASON GREENWOOD (Manchester United)**

Mason Greenwood, ambaye anatajwa na Alan Shearer kwamba anaweza kuvunja rekodi yake ya kufunga mabao kwenye Ligi Kuu England, alikuwa na msimu wa kuvutia zaidi uliopita.

Greenwood alionekana kufanya vizuri katika kila nafasi aliyopewa kwenye kikosi cha Manchester United. Akiwa na umri wa miaka 18 aliweza kufunga mabao 10 kwenye Ligi Kuu England na ukiangalia umri wake ni wazi kwamba ana nafasi kubwa zaidi ya kutamba kwa msimu huu.

Msimu huu mashabiki watakuwa na shauku kubwa ya kumwona Greenwood akiwa kwenye ubora wake.

**2-NICOLAS PEPE (Arsenal)**

Nicolas Pepe hakuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu uliopita.

Ulikuwa wakati mgumu kwake katika mwanzo wake wa kucheza kwenye Ligi Kuu England. Alinunuliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 72.

Kiasi hicho cha fedha kiliwapa matarajio makubwa zaidi mashabiki wa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast angeweza kile wanachokitaka.

Lakini alifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho sita kwenye mechi 31 za Ligi Kuu England alizocheza msimu uliopita. Pepe alishindwa kuwa kwenye ubora wake kama alivyotamba alipokuwa nchini Ufaransa.

Hata hivyo, mwishoni mwa msimu uliopita mashabiki wa Arsenal walianza kuona ubora wa Pepe hasa baada ya kuwasili kwa kocha, Mikel Arteta.

Hivyo basi, bila shaka yoyote, msimu huu unaweza kuwa bora zaidi kwa Pepe na wengi wanasubiri kuona mazuri kutoka kwake.

**1- KAI HAVERTZ (Chelsea)**

Wakati klabu kubwa zinapokugombea kwa kipindi chote cha majira ya joto, ni wazi umeonyesha ni mchezaji mwenye kiwango cha aina yake.

Kai Havertz ni mmoja ya wachezaji vijana ambao wanatarajiwa kutamba zaidi katika soka la Ulaya kwa siku za usoni na sasa raia huyo wa Ujerumani ametua kwenye kikosi cha Chelsea.

Licha ya kuwa na umri wa miaka 21, Havertz alifunga mabao 77 katika mechi 150 alizoichezea Bayern Leverkusen. Hivyo wengi wanatarajia kumwona aking'ara zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Chelsea ilikamilisha usajili wa Havertz, Septemba 4, mwaka huu kwa dau la pauni milioni 71. Kiasi hicho cha fedha kwa mchezaji mwenye umri wa miaka 21 kitamfanya kuwa na presha kubwa kwake. Hivyo mashabiki wengi wa Chelsea wanatarajia kumwona Havertz akitamba chini ya kocha, Frank Lampard.

# VIUNGO 10 BORA ZAIDI KARNE YA 21

**LONDON,** England

KUJARIBU kuwataja viungo bora katika karne ya 21 sio kazi rahisi. Tumeshuhudia viungo wengi wakali katika kila upande wa duniani kwenye mchezo wa mpira wa miguu.

**Lakini pamoja na yote, kuna wakali zaidi ya wengine ukiamua kuwaweka kwenye orodha. Makala hii inakuchambulia viungo 10 bora zaidi kwa karne ya 21.**

### 10- XABI ALONSO

Xabi Alonso alikuwa mmoja wa viungo wa kipekee kwenye soka mwenye ubunifu wa aina yake katika kutengeneza pasi na kukaba. Alikuwa kiungo muhimu katika kikosi cha Hispania wakati kilipotawala soka la dunia. Amecheza katika klabu za Liverpool, Real Madrid na Bayern Munich.

Alonso amefunga mabao mengi ya aina yake na ameshinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Liverpool na Real Madrid na ameshinda mataji ya Ligi Kuu akiwa na Los Blancos na Bayern Munich.

Alonso alikuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Hispania wakati ikishinda Kombe la Dunia mwaka 2010, na ni mmoja wa viungo bora zaidi katika kizazi chake.

### 9- LUKA MODRIC

Luka Modric ni mmoja wa viungo ambaye ameshinda tuzo ya Ballon d'Or. Ndiye aliyevunja umwamba wa Cristiano Ronaldo na Lionel Messi katika tuzo hizo. Modric aliwasili Real Madrid akitokea Tottenham na alikuwa na wakati mgumu katika siku zake za mwanzo.

Lakini raia huyo wa Croatia haraka alizoea soka la Hispania na kuwa kiungo muhimu zaidi kwa Real Madrid.

Modric alikuwa nguzo wakati Real Madrid wakitawala kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakilibeba taji hilo mara tatu mfululizo.

### 8- FRANK LAMPARD

Pengine ndiye kiungo bora zaidi mwenye uwezo wa kufunga, Frank Lampard na ni mmoja wa wachezaji wa Uingereza mwenye uwezo wa aina yake. Alifunga mabao 211 kwa Chelsea wakati akicheza nafasi ya kiungo.

Mwingereza huyo ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu, moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, moja la Ligi ya Europa, matano ya Kombe la FA na matatu ya Ligi.

Lampard pia alikuwa na uwezo mkubwa wa kufunga kwa mashuti ya mbali akiwa nje ya eneo la 18.

### 7- STEVEN GERRARD

Steven Gerrard ni mmoja wa viungo wenye staili ya kipekee kwenye uchezaji. Aliamua kuwa mtiifu kwa Liverpool na kucheza pale kwa karibia kipindi chake chote cha uchezaji soka.

Gerrard alijulikana kwa uwezo wake wa kufunga magoli kwa mashuti makali na pia kucheza kama mshambuliaji.

Alikuwa nahodha wakati akiiongoza Liverpool kupindua matokeo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakiwa nyuma kwa mabao 3-0 dhidi ya AC Milan kule jijini Istanbul, Uturuki.

Pamoja na yote, Gerrard hajawahi kushinda taji la Ligi Kuu England na ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara moja, mawili ya FA na matatu ya ligi.

### 6- KAKA

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa hazuiliki wakati akiwa kwenye ubora wake pale AC Milan. Huyu ni mchezaji wa mwisho wa Brazil kushinda tuzo ya Ballon d'Or kabla ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kuingia kwenye zama ya kupokezana kwa karibu miaka 10.

Usajili wa fedha nyingi kwenda Real Madrid hakukuwa na mafanikio kwake, kwani hakutamba tangu kuondoka kwake kule Rossoneri.

Kati ya mwaka 2006 na 2009, alitajwa kwenye kikosi cha FIFA na UEFA mara tatu.

Kaka alishinda Kombe la Dunia akiwa na Brazil mwaka 2002 na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na AC Milan msimu wa 2006-07. Pia alishinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, na La Liga.

### 5- PAUL SCHOLES

"Anatosha kuichezea Brazil. Napenda kumwangalia Scholes, akipiga pasi, kijana mwenye nywele nyekundu na jezi nyekundu." - Maneno ya Socrates.

"Bila shaka yoyote mchezaji bora kwenye Ligi Kuu England anapaswa kuwa Scholes ... anajua kila kitu." - Kauli ya Thierry Henry.

"Ni mtu anayenivutia. Kwa uhakika kabisa ni mmoja wa viungo bora kabisa duniani. Wachezaji wanampenda." Kauli ya Xavi.



MODRIC

Kauliza hapo juu kutoka na magwiji hao wa soka inaonyesha namna gani Scholes alivyokuwa kiungo wa aina yake dimbani. Alikuwa injini ya Kocha 'Sir' Alex Ferguson pale Old Trafford.

Scholes alishinda mataji 11 ya Ligi Kuu England, mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, manne ya FA na mawili ya Ligi.

### 4- ANDREA PIRLO

Ni rahisi sana kumtambulisha Andrea Pirlo. Mtu ambaye kazi yake ilikuwa moja tu uwanjani kusukumiza mshambulizi mbele na kuituliza timu pinzani pale kwenye dimba la kati.

Pirlo alikuwa nyota kwa klabu zote kubwa za Italia, Inter Milan, AC Milan na Juventus na alikuwa nguzo ya mafanikio ya kikosi cha Timu ya Taifa ya Italia kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2006.

Ameshinda mataji sita ya Serie A - mara mbili akiwa na AC Milan na mara nne akiwa na Juventus. Alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Milan. Pirlo alikuwa nyota wa mchezo kwenye fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2006 dhidi ya Ufaransa na Italia ikatwaa kombe.

### 3- ZINEDINE ZIDANE

Kuna mengi sana unaweza kuyataja kwa Zinedine Zidane ambaye ni mmoja wa viungo wakali zaidi kutokea katika sayari hii.

Alitajwa mchezaji bora wa mwaka wa Fifa mara tatu, mwaka 1998, 2000 na 2003.

Zizou pengine ndio mchezaji bora zaidi wakati akiichezea Timu ya Taifa ya Ufaransa na alishinda Kombe la Dunia mwaka 1998 na lile la mataifa ya Ulaya mwaka 2000.

### 2- XAVI

Xavier Hernandez au Xavi ni mmoja wa wachezaji bora kabisa waliozalishwa na kituo cha kulelea vipaji cha La Masia. Mkali wa pasi na injini ya Barcelona na Hispania wakati akizichezea timu hizo.

Xavi ameshinda mataji mengi akiwa na Barcelona na Hispania. Alikuwa mmoja kwenye kikosi cha Barcelona kilichoanzisha staili ya mchezaji wa tiki-taka mfumo ulioanzishwa na Johan Cruyff.

Xavi ameshinda mataji nane ya La Liga, mataji manne ya Ligi ya Mabingwa ULaya, Kombe la Dunia na Hispania na Kombe la Mataifa ya Ulaya mara mbili mwaka 2008 na 2012.

### 1- ANDRES INIESTA

Andres Iniesta huyu alikuwa patina mzuri wa Xavi katika nafasi ya kiungo ya Barcelona na Hispania akishinda mataji tisa ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku pia akibeba Kombe la Dunia mwaka 2010 na lile la mataifa ya Ulaya mwaka 2008 na 2012.

Iniesta ni mmoja wa viungo bora zaidi katika historia ya soka duniani. Ni kiungo mwenye ubunifu wa aina yake.

Hadi sasa anatajwa kama kiungo asiye na mfano wake katika soka na kuwa mchezaji ambaye mpira ulimheshimu zaidi ukifika miguuni mwake.

## Nukuu

"Mara ya kwanza wakati nilipojiunga na Arsenal, sikuwa na uhakika kabisa, kiukweli hatukuwa vizuri kifedha na ndio nikaona uwezekano wa Aubameyang kubaki ni mdogo sana. Lakini hatimaye mambo yakaenda sawa na sasa amebaki na atakuwa na sisi kwa miaka mingine mitatu." **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alisema.**



"Miezi minne hadi mitano kwa mchezaji bila ya kucheza ni mingi sana, Carlinhos (Carlos) na Yocouba (Sogne) ni wachezaji wazuri na wana uwezo mkubwa, wataisaidia timu kupata matokeo lakini bado kwangu hawajawa fiti kuwapa muda mrefu wa kucheza," **alisema Kocha wa Yanga, Zlakto Krmpotic.**



"Nilikuwa na wakati mzuri sana wa kuwa hapa Arsenal na sasa natakiwa kuondoka sehemu ambayo ilikuwa nyumbani, asante sana kwa sapoti yenu. Nimekaa miaka 11 na klabu hii na kwa hakika ulikuwa wakati wa furaha zaidi na sijawahi kujutia kucheza hapa." **Golikipa Emiliano Martinez, alisema ambaye amejiunga na Aston Villa.**






# MAPROO WALIVYOING'ARISHA YANGA LIGI KUU BARA

**Mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons kutoka Mbeya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikaifunga Mbeya City kwenye uwanja huo huo, kabla ya Jumamosi iliyopita kushinda kwa mara ya kwanza ugenini bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar.**

**Na Adam Fungamwango**

MPAKA wakati huu, Yanga imecheza mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa imeshinda michezo miwili na kutoka sare moja, ikicheza mechi mbili nyumbani na nyingine ugenini.

Imejikusanyia pointi saba, magoli matatu, ikiwa imefungwa bao moja.

Ukiangalia timu hiyo mpaka kufikia raundi ya tatu imebebwa zaidi na wachezaji wa kigeni zaidi.

Ni wale iliyowasajili msimu huu na wale waliokuwapo awali.

Mpaka sasa ambapo Yanga ina magoli matatu, yote yamefungwa na wachezaji wa kigeni, huku kukiwa hakuna mchezaji yoyote wa Kitanzania aliyefunga goli kwenye timu hiyo.

Kwenye makala haya, tunaangalia mchango wa wachezaji kutoka nje ya nchi kwenye mechi tatu zilizocheza.

**MICHAEL SARPONG (Yanga 1-1 Prisons)**

Huyu ni raia wa Ghana na ndiye mchezaji wa kwanza wa Yanga kufunga msimu huu kwenye Ligi Kuu.

Alifanya hivyo dakika ya 18 kwenye mechi dhidi ya Tanzania Prisons. Wakati huo tayari Prisons ilikuwa imeshapata bao moja kupitia kwa Lambart Subianka.

Ilitokea hekaheka kwenye lango la Prisons, kutokana na mpira uliokokotwa na Farid Mussa, alipiga krosi iliyookolewa vibaya na mabeki wa Prisons.

Sarpong, straika aliyesajiliwa msimu huu akitokea Rayon Sport ya Rwanda, aliukuta mpira ukiwa unazagaazagaa akaujaza wavuni na mechi hiyo ikaisha kwa sare ya bao 1-1, akawa ameiokoa Yanga na kipigo.

Mechi hiyo ilichezwa Septemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**LAMINE MORO (Yanga 1-0 Mbeya City)**

Beki wa kati, Lamine Moro aliipatia Yanga bao pekee kwenye mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Septemba 13, mwaka huu.

Lamine pia ni raia wa Ghana, akiwa mmoja wa wachezaji wa kigeni walioing'arisha Yanga kwenye mechi za Ligi Kuu mpaka sasa.

Ilikuwa ni dakika ya 85, baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga wakiwa wameshaanza kutoka uwanjani wakiwahi usafiri, wengine kwenye magari yao binafsi, kila mmoja akidhani mechi ingeenda sare, mambo yalibadilika.

Ilikuwa ni kona wa mchezaji mwingine mpya wa kigeni, Carlos Carlinhos kutoka Angola, iliyokwenda kutua kwenye kichwa cha mchezaji huyo wa kigeni ambaye yupo kwa msimu wa pili sasa, Lamine akaukwamisha wavuni.

Ni bao lililowafanya Yanga kutoka uwanjani na ushindi wa bao 1-0, ikipata pointi tatu na kuifanya kuongeza na kufikia ponti nne.

**MUKOKO TONOMBE (Yanga 1-0 Kagera Sugar)**

Ni mechi juzi Jumamosi ambayo mchezaji mwingine wa kigeni, Mukoko Tonombe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), aliifungia Yanga bao dakika ya 72 na kuifanya timu hiyo kutoka uwanjani na ushindi wa bao 1-0, kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Ni mechi ya kwanza kushinda ikiwa ugenini. Mukoko alifunga bao hilo pekee akipata pasi maridadi kutoka kwa Mkongomani mwenzake, Tuisila Kisinda ambaye alimtambuka, Ally Sonso wa Kagera Sugar kwenye winga ya kulia, akaingia ndani na kutoa pasi kwa mfungaji ambaye aliugusa mara ya kwanza, kabla ya kuachia shuti la juu lililojaa wavuni na kushinda kipa Ramadhani Chalamanda.

Yanga ambao msimu huu hawashiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wataendelea kucheza ugenini, ambapo Septemba 27, mwaka huu watawafuata Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

**JE, WAJUA?**



RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Leodegar Tenga ambaye kwa sasa ni Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya FIFA (TSG) na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Nchini (BMT), aliichezea kwa mafanikio Timu ya Taifa (Taifa Stars) kati ya mwaka 1975 na 1981. Baada ya hapo aliteuliwa kuwa meneja wa klabu ya Pan African hadi mwaka 1984.



# Makusanyo kuwapima mameneja Posta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Shirika la Posta Tanzania, imetakiwa kuweka vigezo maalum vya kupima utendaji kazi wa mameneja wa mikoa kwenye makusanyo, ili watakaoshindwa kukidhi waondolewe.

Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga mafunzo kwa viongozi wa shirika hilo nchini yaliyofanyika kwa siku tano, jijini hapa.

Alisema kila tawi la shirika hilo lihakikishe linapata faida na washindane kwa kadri faida inavyotengenezwa ili kuongeza gawio kwa serikali.

"Yawekwe malengo wafanyie kazi, yaani kwa mfano mtu yupo tawi la kati kati ya mji, kwa mwaka awekewe zikusanywe Sh. milioni 350 faida, haijalishi wewe utafanya nini, kama hujafikisha utapaswa kutupisha aje mwingine ndivyo wanavyofanya," alisema.

Aliongeza: "Hili gawio la Sh. milioni 350 kwa ukubwa wa shirika hili, haiwezekani, tunatarajia kwa muda mfupi ujao tuanze kuzungumzia bilioni na tunajua inawezekana."

Hata hivyo, alisema kuna kamati yake ya ufundi inatengeneza mikataba ambayo itakuwa na malengo ya kupima shirika hilo.

"Tunataka tukikupima tukupime kwa kitu sahihi, katika muda mfupi ujao mtapata na kusaini mikataba mipya ili kuhakikisha kwamba Shirika la Posta linafanya kwa ufanisi kulingana na vigezo vya kupima ufanisi," alisema.

Mbuttuka alipongeza shirika hilo kwenye faida hasi na kuwa na faida chanya.

"Tuseme ukweli kwamba bado kazi kubwa inahitajika, pamoja na pongezi hizi kuna maeneo tunatarajia kuona kwa shirika linazingatia, kwa miaka mitatu mfululizo limejitahidi kutoa gawio, miaka miwili mmetoa Sh. milioni 350, ule mwaka mwingine mmetoa Sh. milioni 250, mnajua haitoshi," alisema.

Msajili huyo alisema vimewekwa vigezo vya gharama za uendeshaji ambapo zinatakiwa zisizidi asilimia 50 lakini bado shirika linajiendesha kwa gharama ya asilimia 75.

Aidha, alisema katika biashara ya usafirishaji wa sampuli za damu shirika limeaminiwa na serikali kupewa jukumu hilo kwa ustawi wa nchi na kuwataka kuwa makini na serikali kuendelea na imani hiyo.

Akizungumza kuhusu mafunzo, alisema kama shirika limeweka mikakati yake ya utendaji kazi lazima lijipange kuwa na uwezo wa kushindana na ubunifu unahitajika zaidi.

"Kama hatutaweza kukabiliana na vikwazo vya soko, kubadilika kuendana na soko na hatutaongeza kasi kwenye utendaji kazi, washindani wetu watatushinda, mafunzo haya ni muhimu kwa maslahi mapana na uhimilivu wa shirika letu," alisema.

Alibainisha kuwa mafanikio watakayopata yatategemea namna ya kutekeleza wajibu wao.

Alikemea migogoro sehemu ya kazi kwa kuwa imekuwa ikirudisha nyuma utendaji wa shirika.

Naye, Posta Masta Mkuu wa Shirika hilo, Hassan Mwang'ombe, alisema shirika hilo liliweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa viongozi wa juu ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Alisema mafunzo hayo yameweka mwelekeo mmoja wa utendaji kazi ambapo kuna viwango vya ufanisi vimewekwa ambapo kila Meneja wa Mkoa anatakiwa awe amezalisha asilimia 75 ya bajeti ya shirika.

"Tumeweka viwango ambavyo tutasimamia ili kufikia malengo tunayoyataka. Sisi tumeangalia na kuweka vigezo na mikakati ambayo itasaidia kufikia lengo la kuwa vinara wa utoaji huduma za usafirishaji," alisema.

Aidha, alisema kutokana na mikakati hiyo wanatarajia kuongeza utoaji wa gawio kwa serikali.



Maofisa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakiangalia ramani ya eneo la Kisasa katika Jiji la Dodoma kabla ya kuanza zoezi la Siku ya Mlipakodi, ambapo walitembelea nyumba kwa nyumba kwa lengo la kuhamasisha ulipaji kodi ya ardhi sambamba na kusikiliza changamoto za sekta ya ardhi mwishoni mwa wiki jijini humo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Mwongozo kuwasaidia wabunge kusimamia maamuzi ya serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KITUO cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB), kimeanda mwongozo wa kuwasaidia wabunge katika kusimamia maamuzi mbalimbali yanayofanywa na serikali kwenye utekelezaji wa miradi ya umma.

Meneja mradi wa kituo hicho, John Kitoka, alibainisha hayo jana mara baada ya kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa masuala ya manunuzi na mikataba ya umma.

Kitoka alisema kuwa hiyo ni kutokana na utafiti mdogo waliofanya wamebaini kuwa wabunge wengi hawajui taratibu na kanuni na sheria za usimamizi wa umma.

Alieleza kuwa mwongozo huo utawasaidia kuwaongezea maarifa katika kuisimamia serikali pamoja na kuihoji juu ya miradi mbalimbali inayoitekeleza.

"Mwongozo huu utawasaidia waheshimiwa wabunge kuwafumbua macho na kuhoji serikali namna mbalimbali wanavyotekeleza miradi ya umma kwani wao ndio wawakilishi wa wananchi, hivyo ni vizuri wananchi wakawa wanajua masuala ya maendeleo yanavyofanyika," alisema Kitoka.

Aidha, alisema mwongozo huo utawasaidia wabunge kuhakikisha manunuzi ya umma yanafanyika kwa kufuata taratibu za kisheria na miradi inatekelezwa kwa kuzingatia sheria za manunuzi na michakato yote.

Kwa upande wake, Ofisa Miradi wa TCIB, Annex Moza, alisema kuwa mwongozo huo utawasaidia kuangalia namna wabunge watasaidia serikali kutimiza majukumu yake katika kufanya manunuzi.

"Suala la mikataba mibovu ni sugu katika nchi za Kiafrika na inatokana na mifumo iliyopo ikiwapo usiri na hivyo kusababisha kuwapo kwa mikataba hiyo mibovu isiyotekelezeka na kuisababishia serikali hasara," alisema.

Mshiriki wa mafunzo hayo, Daniel Msangya, alisema manunuzi yanachukua sehemu kubwa ya fedha za serikali, hivyo ni lazima kuwapo mifumo ya wazi na imara ili kudhibiti upotevu wa fedha nyingi za umma.

# Machinga wamuunga mkono Magufuli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAJASIRIAMALI wadogo (Machinga) jijini Dodoma wamesema wanamuunga mkono Rais John Magufuli katika uchaguzi mkuu 2020, kutokana na kuwapatia vitambulisho vya ujasiriamali ambavyo vimewapa uhuru wa kufanya biashara zao.

Akitoa tamko lao jana, Mwenyekiti Msaidizi wa machinga, Bruna Mponzi, alisema vitambulisho hivyo vimeondoa migongano kati yao na serikali na kufanya biashara zao kwa uhuru kwa sasa na kujiingizia kipato tofauti na awali ambapo walikuwa wakikimbizwa ovyo.

"Tunashukuru serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli kwa kuwa mstari wa mbele katika kutatua kero zetu zilizokuwa zikitukabili awali, kila kitu tukiwasilisha kinatatuliwa kwa wakati, Ofisa Masoko James Yuna anafanya kazi kwa karibu na sisi, tunashukuru serikali kwa hatua ambazo inazichukua kwa haraka kwetu," alisema.

Alisema kwa sasa wanakaa meza moja na serikali katika kutatua kero zinazowakabili.

"Machinga wa leo ukiangalia kwa miaka miwili iliyopita kabla kupewa vitambulisho vya ujasiriamali, tulikuwa tunaishi kama paka na chui na serikali, tupo pamoja na Rais John Magufuli na tuna imani tutampigia kura," alisema.

Naye Mweka Hazina wa Machinga, Athuman Ally, alisema wanaamini Magufuli ataendelea kuwasaidia zaidi na atatoa mazuri zaidi kwa ajili ya wafanyabiashara hao.

"Sisi Machinga hatuna jingine la kumpatia, tunachoahidi ni kumpa kura ili aendelee kuweka mambo sawa na kujenga heshima ya Machinga," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Machinga Stendi ya Mabasi Dodoma, Shaban Kisamvu, alisema wanamshukuru Rais Magufuli kwa kujengwa kwa stendi ya kisasa ya Dodoma ambayo ni fursa kubwa kwao kwa kuwa wamerasmishwa kufanya biashara zao.

Mwenyekiti wa Machinga Soko la Sabasaba, Elizabeth Siame, alisema kwa kipindi cha nyuma wajasiriamali wadogo walikuwa wakinyanyasika lakini kwa sasa hawakumbani na kikwazo chochote.

Akipokea shukrani hizo, Kaimu Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, alishukuru machinga kwa kuthamini kazi iliyofanywa na Rais Magufuli kwa kuwawekea mazingira mazuri ya utendaji kazi.





# SHIVYAWATA yataka ulegezaji wa masharti ya utoaji wa mikopo

**Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Mbeya, limeiomba serikali kuangalia upya masharti ya utoaji mkopo wa asilimia mbili kutoka halmashauri ili kundi hilo linufaike na kumudu gharama za maisha.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti Shirikisho hilo mkoani hapa, Luca Mahenge, wakati akizungumza na Nipashe namna serikali imewawezesha kujikwamua na umaskini kupitia mikopo.

Mahenge alisema serikali iangalie upya utaribu wa utoaji mikopo kwa kundi hilo kwa kuhakikisha wanarekebisha baadhi ya sera na sheria ambazo zinamnyima haki mwenye ulemavu kukopesheka.

Akizungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB), mkoani Mbeya, Joseph Mwandalima, alisema licha ya serikali kutoa fursa ya mikopo, lakini bado kuna mlolongo mrefu wa kupata mikopo hiyo kutokana na masharti yaliyowekwa.

Alisema masharti yaliyowekwa na halmashauri yamekuwa magumu kwao, hali inayosababisha kukosa sifa ya kukopesheka hivyo wanaiomba serikali kuangalia upya ni kwa namna gani watalisaidia kundi hilo.

"Miongoni mwa masharti ambayo halmashauri zetu imeweka kwenye mikopo yao ni kwamba kila kikundi lazima wapate usajili na barua kutoka kwa watendaji wa vijiji... sisi wenye ulemavu tumetawanyika unashangaa wawili wako kijiji kimoja na wengine wako mbali, sasa ni ngumu kuunganika kwa pamoja cha muhimu watuhimize tujisajili bila kujali tunatoka kijiji kimoja," alisema Mwandalima.

Aliongeza kuwa licha ya vikwazo walivyonavyo, aliwahamasisha wenzake kuendelea kuchapa kazi kwa kufanya shughuli ndogo ndogo za kujiingizia kipato.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu (CHAWATA), Mkoa wa Mbeya, Jimmy Ambilikile, alisema msaada kwa sasa kundi hilo sio tegemezi tena kwani wameanzisha shughuli ambazo zinawaongezea kipato, lakini hitaji lao ni mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za kifedha na halmashauri.

# RC awaomba viongozi dini kuombea uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema taifa litakuwa katika mikono salama endapo viongozi wa dini wataendelea kusimama imara katika kuombea mchakato wa Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba 28, mwaka huu, umalizike salama kwa kuwachagua viongozi bora.

Aidha, aliwasihi waendelee na maombi ili taifa liweze kupata kiongozi sahihi atakayehakikisha Tanzania inaendelea kuwa nchi inayodumisha amani, upendo na utulivu pamoja na kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Chalamila alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na viongozi wa dini kwa lengo la kujadili ni kwa namna gani viongozi wa dini wana mchango katika kudumisha amani na utulivu kupitia mahubiri yao kuelekea uchaguzi mkuu.

Alisema katika kufanikisha hayo, viongozi wa dini wanapaswa kufunga na kuomba ili kuweza kupata kiongozi sahihi ambaye atawaunganisha pamoja na kuwaletea maendeleo.

Aliongeza kuwa madhara ya kumchagua kiongozi asiye muadilifu kwa madai kuwa anaweza kugharimu maisha ya watu, lakini pia kujinufaisha peke yake.

"Madhara ya kupata kiongozi asiyekuwa na hofu ya Mungu anadhani tumeyaona hata kwa baadhi ya viongozi katika maeneo, viongozi wa dini mna jukumu la kuwahubiria watu kumjua Mungu, ili anayehitaji uongozi afahamu kabisa amebeba dhamana kubwa ya kuwaletea maendeleo wananchi," alisema Chalamila.

Viongozi wa dini wameapa kuwa mabalozi wa kuhubiri amani na utulivu kwa waumini wao kwa kuhakikisha uchaguzi ujao unafanyika vyema sambamba na kuwahubiria kuwachagua viongozi watakaowaletea maendeleo.

Akiwa mkoani Mbeya, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, aliwaomba wagombea wote ambao majina yao hayakurudi kutoa ushirikiano kwa wagombea waliosimamishwa na chama hicho ili kushinda kwa kishindo.

Alisema licha ya CCM kujipambanua kwa shughuli za maendeleo walizozifanya kwa wananchi, lakini wagombea wanapaswa kunadi sera za Ilani ya CCM za mwaka 2020/2025, ambazo zimesheheni masuala mbalimbali ya kuwaletea wananchi maendeleo.




Wafanyakazi wa baa ya Break Point mkoani Mbeya, wakiwa na mabango yenye ujumbe wa unywaji kistaarabu yaliyotayarishwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) wakati wa kuadhimisha Siku ya Unywaji Kistaarabu Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge mteule aahidi utatuzi wa kero

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE mteule wa ubunge viti maalum Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, amedai kuwa endapo wakazi wa Jimbo la Mbeya Mjini watakipa ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuongoza jimbo hilo watahakikisha wanatatua kero zote zinazowakabili zikiwamo za sekta ya elimu, afya, maji, kilimo na miundombinu.

Mahundi aliyasema hayo juzi wakati wa kampeni za kumnadi mgombea wa chama hicho, Dk.Tulia Ackson, kwenye maeneo ya kata mbalimbali za Jiji la Mbeya. Alisema wananchi wakiipa kura CCM watafurahia maisha kwa sababu wataboreshewa huduma mbalimbali za kijamii.

"Katika kampeni zetu tumeweleza wananchi kwa endapo wakitupa nafasi tutatua matatizo yao, lakini tumewahimiza kumpigia kura za mfano Rais John Magufuli kwa sababu ya mambo makubwa aliyotufanyia, hakuna ambaye hajayaona uboreshaji katika sekta ya elimu, maji, afya, mikopo, miundombinu ya barabara, meli, reli na anga," alisema Mahundi.

Alidai kuwa kipindi cha miaka 10 ambacho jimbo hilo lilikuwa mikononi mwa upinzani, hakuna maendeleo yaliyofanyika.

Aidha, mbunge huyo aliwaomba kinamama kukupigia CCM kwa madai kuwa kimebeba ajenda ambazo zimelenga kumsaidia kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo, vipaumbele vya ajira na fursa za kibiashara.

Mgombea udiwani kwa tiketi ya CCM Kata ya Majengo, Maulid Issa, alisema moja ya vipaumbele vyake ni kuboresha mazingira ya utoaji mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, kulegeza masharti ambayo miongoni ni kuhimiza wahitaji lazima wawe na shughuli za kufanya kwanza ndipo wapate mikopo.

Aliongeza kuwa kazi kubwa atahamasisha wanawake kujiunga na vikundi mbalimbali vya ujasiriamali na kwamba atakuwa anatoa kiasi cha fedha ili kuongeza uzalishaji.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliwaomba wananchi kufanya uchaguzi sahihi wa wagombea kwa kuhakikisha wanamchagua mtu makini ambaye ataweza kubeba ajenda zao na kuzisemea kwenye vyombo vya maamuzi.





# Shein ataja mchango sekta binafsi kupaa kwa uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa serikali anayoiongoza imeamua kushirikiana na sekta binafsi kwa kuwa ndio injini ya uchumi wa nchi.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa Jukwaa la 11 la Biashara lililofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil, Kikwajuni jijini Zanzibar ambalo lilitanguliwa na Baraza la Taifa la Biashara lililofanyika Ikulu Zanzibar.

Dk. Shein alisema kuwa uchumi unakua kutokana na kuwapo kwa sekta binafsi na serikali imeamua kwa makusudi katika kuhakikisha hilo linafanikiwa na tayari mafanikio makubwa yameshaanza kupatikana.

Alisisitiza kuwa umoja uliojengwa na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi ni lazima uimarishwe zaidi na faida kubwa itaendelea kupatikana.

Rais Dk. Shein ambaye alikuwa ni mwenyekiti wa jukwaa hilo, alisema kuwa kukutana huko ni ahadi yake ya kwa lengo la kuagana baada ya kufanya kazi nzuri kwa kipindi cha karibu miaka tisa.

Aliupongeza uongozi wa Wizara Biashara na Viwanda kwa kusimamia suala zima la biashara katika kituo cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati tokea karne ya 16.

Dk. Shein alieleza historia ya Zanzibar katika biashara, ambapo biashara zilitoka nchi ya nje zikiwamo Uingereza, India, Hong Kong na nchi nyinginezo, huku akisisitiza kuwa Zanzibar si mwanagenzi wa biashara.

Aidha, alisema kutokana na kuwapo kwa changamoto ya kibiashara hivyo, ni vyema biashara ikatangazwa.

Pia Dk. Shein alisema kuwa vikao vya baraza hilo vilivyokuwa vikifanyika vilikuwa vikieleza suala zima la biashara na uchumi pamoja na uwekezaji.

"Tulikuwa tukijadili kwa hoja na kila mmoja aliweza kutoa maoni yake hali ambayo ilisaidia kuimarisha biashara...na leo hakuna tofauti ya sekta ya biashara na sekta ya umma, sote watu wamoja, ndivyo tulivyofanya miaka tisa iliyopita," alisema Dk. Shein.

Naye Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alipongeza mafanikio yaliopatikana katika kuimarisha Sekta ya Biashara chini ya uongozi wa Rais Dk. Shein.

Alisema kuwa serikali imeweka Jukwaa la Biashara ambalo limekuja na kaulimbiu ya "Mazingira rafiki ya ufanyaji biashara kwa maendeleo ya Zanzibar" ambayo imekuja baada ya kufanyika taratibu zilizowekwa na serikali kutokana na mazingira ya dunia. Alisema serikali imefanya utafiti wa mwaka 2020 ambapo pia hivi sasa Zanzibar imekuwa ya 101 katika eneo la urahisi wa biashara.

Alisema ndani ya miaka kumi mambo mengi yamefanywa katika eneo la biashara na viwanda, mambo mengi ya msingi yamefanyika ila juhudi zaidi zitafanyika katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa kituo cha biashara.

Rais wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar,Taufiq Turky, alimpongeza Rais Dk. Shein kwa kusimamia vyema uchumi hasa katika kipindi cha janga la corona ambapo licha ya bidhaa kupanda bei duniani, lakini kwa upande wa Zanzibar haikuwa hivyo.

Alisema katika historia kiongozi msikivu, mwenye hekima, busara na kuwasiliza wananchi wake, huku akisema kuwa Rais Dk. Shein amefanya mambo mengi na wafanyabiashara wataendelea kumkumbuka.

Alieleza kuwa jumuiya hiyo imeweza kushirikiana na jumuiya mbalimbali za kimataifa zikiwamo nchi za Uturuki, China, Dubai, Qatar, Moroco na nyinginezo.



WanaCCM na wapenzi wa chama hicho wakimshangilia mgombea wa uwakilishi visiwani Zanzibar, Mohamed Ahmada Salim, anayetetea nafasi hiyo alipoelezea mambo aliyoyafanya miaka mitano ya uwakilishi wake. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Spika apigia debe wagombea CCM

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, amewataka wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kuwachagua viongozi wa jimbo hilo, kupitia CCM ili chama hicho kiweze kupata tena ushindi katika uchaguzi mkuu.

Alisema kuna kila sababu kuwachagua tena wagombea wa jimbo hilo kupitia CCM ili kumalizia changamoto zilizopo.

Alisema kuwa viongozi hao akiwamo mbunge na mwakilishi wa jimbo hilo ambao wanatetea tena nafasi hizo, wamefanya mambo makubwa ikiwamo kutatua kero ya maji jimbo humo.

Naye mgombea ubunge wa Jimbo la Kikwajuni, Hamad Yussuf Masauni, alisema heshima waliyompa ni kubwa mno kwa muda wa miaka 10 na hawatawaangusha katika miaka mitano ijayo endapo atapata ridhaa za wananchi wa jimbo hilo kuwa mbunge.

Alisema kipaumbele chake katika awamu hii ni kupambana na changamoto ya ajira kwa vijana.

Alieleza kuwa atawaendeleza kielimu vijana katika sekta ya uvuvi, ili wasiwe nyuma katika uchumi wa bahari.

Alisema pia atawajengea mazingira mazuri vijana ili kuwa na ushindani katika ajira.

Kwa upande wake mgombea uwakilishi wa jimbo hilo, Nassor Jazira, alisema kuwa endapo atapata ridhaa za wananchi, ataendelea kuwaletea maendeleo.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Wilaya ya Mjini, Borafya Silima, aliwataka wana CCM ambao waligombea lakini hawakupata wasinune na wakisamehe chama chao pale ambapo mtu hajaridhika na uteuzi na sasa kuwa kitu kimoja.

# SMZ kujenga vyuo zaidi vya ufundi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema itaendelea kujenga miundombinu bora na ya kisasa ya vyuo vya Amali (ufundi) ili kuwapatia fursa wanafunzi kukuza ujuzi wao.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrissa Muslim Hija, alieleza hayo katika sherehe ya ufunguzi wa maonyesho ya ufundi na kazi za amali katika viwanja vya mnara wa Kumbumbuku Mapinduzi Square, Kisonge Mjini Unguja.

Alisema kujenga vyuo hivyo kutasaidia kupunguza vijana wanaosubiri ajira kutoka serikalini na badala yake wajiajiri wenyewe kutokana na ujuzi watakaoupata.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa fursa hata kwa taasisi binafsi kutoa taaluma ya ufundi na ujasiriamali kwa lengo la kuwakwamua vijana kutoka katika mazingira ya utegemezi, ili Taifa liweze kupata maendeleo zaidi.

Aidha, aliwasisitiza wanafunzi kuhakikisha kuwa wanatumia vizuri fursa ya kupata ujuzi katika vituo mbalimbali vya amali vilivyosajiliwa nchini ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Naye Naibu Katibu Mkuu Taaluma wa wizara hiyo, Madina Mjaka Mwinyi, aliwataka wazazi kuwapa fursa watoto wao ya kushiriki michezo mbalimbali ambayo ni sehemu ya masomo yao, ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kuwa na ufahamu wa masomo yao.

Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo ya Amali, Dk. Bakari Ali Silima, alisema kutokana na dunia kuwa na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona ipo haja ya kuwandaa vijana kujiajiri wenyewe kwa kujenga vyuo vya amali na kuboresha elimu ya ufundi na ujasiriamali nchini ili kusaidia kupunguza tatizo hilo.

Maonyesho hayo ya ufundi na kazi za amali ni miongoni mwa shamrashamra za kuelekea miaka 56 ya elimu bila ya malipo yanayotarajiwa kufikia kilele chake Septemba 23, mwaka huu.

# Mfumo wa kielektroniki waongeza makusanyo NSSF

**Na Mwandishi wetu**

MATUMIZI ya mfumo wa kielektroniki wa malipo ya serikali (GePG), katika Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), umeongeza ukusanyaji wa mapato na kuvunja rekodi ya ukwasi kutoka Sh. Trilioni 3.2 hadi Trilioni 4.4 kwa miaka miwili.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Willium Erio, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa kupokea taarifa ya matokeo ya matumizi na tathmini ya mfumo wa GePG, ambao pia umeongeza ukusanyaji wa makusanyo ya michango kutoka kwa wanachama kutoka Sh. bilioni 694 kwa mwaka na kufikia Sh. trilioni 1.1 Juni mwaka huu.

Alisema mfumo huo ulianza kutumika Aprili, mwaka jana, kwa ajili ya kukusanya michango kwa wanachama kutoka sekta rasmi na sekta isiyo rasmi pamoja na kukusanya kodi ya pango kwa wapangaji waliopanga kwenye vitenga uchumi vya shirika hilo.

Aidha, alisema mfumo huo umeliletea shirika mafanikio makubwa ikiwamo kuongeza mapato kutoka kwa wanachama, ambapo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita ilikuwa ni Sh. bilioni 694 kwa mwaka, lakini katika kipindi hiki hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, yamekaribia Sh. trilioni 1.1, ongezeko ambalo ni kubwa katika kipindi kifupi lililochangiwa na matumizi ya GePG.

Kwa mujibu wa Erio, mfumo huo umesaidia kuondoa ahadi hewa za malipo, na kwamba kabla ya mfumo huo kulikuwa na akaunti za benki 78, lakini baada ya mfumo huu zimeondolewa na kubaki tatu,

"Kuondoa akaunti nyingi kumepunguza makato kutoka Sh. milioni 9.5 kwa mwezi hadi kufikia Sh. milioni 4 kwa mwezi na umeweka uwazi," alisema.

"Hii GePG imeleta mabadiliko makubwa pale NSSF, imeongeza thamani ya mfuko kwa zaidi ya asilimia 40 ndani ya kipindi cha miaka miwili ni kutokana na matumizi ya mfumo huu," alifafanua.

Aidha, alisema mfumo huo umelisaidia sana shirika hilo kwa kuongeza mapato, kupunguza gharama za uendeshaji ambazo walikuwa wanatumia katika matumizi ya kawaida na kuwawezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama na kwa wakati.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alipongeza shirika hilo na kwamba mashirika mengine yanapaswa kuiga.

Alisema yameongeza kiwango cha makusanyo tangu mfumo huo ulipoanzishwa mwaka 2017, kwamba takwimu za maduhuli yaliyokusanywa mwaka wa fedha 2015/16, serikali ilikuwa inakusanya kwa mwaka maduhuli ya Sh. bilioni 688.7.

Alisema makusanyo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 688.7 mwaka 2019/2020, hadi Sh. trilioni 2.699, kwamba katika mwaka huu wa fedha 2020/21, wanatarajia kukusanya zaidia ya kiasi hicho cha fedha.

"Ukiangalia mwaka wa fedha 2015/16 na 2019/20, tumeongeza ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kwa asilimia 292 kiasi ambacho ni kikubwa sana," alisema James.

# Mifugo yahatarisha Hifadhi ya Ruaha

**Na Beatrice Shayo,** MBEYA

HIFADHI ya Taifa ya Ruaha Kanda ya Kusini inakabiliwa na changamoto ya wafugaji kuingiza mifugo katika hifadhi hiyo, hali ambayo inahatarisha usalama wa wanyamapori.

Hayo yalisemwa na Kamshina Msaidizi wa Hifadhi Kanda ya Kusini, Pius Mzimbe, akihojiwa na waandishi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) katika ziara iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Mzimbe alisema moja ya changamoto kubwa ambayo inawakabili ni wafugaji hao kuingiza mifugo ndani ya hifadhi wakiamini kuwa chakula kilichopo kwenye hifadhi hiyo kinanenepesha mifugo yao.

Alisema athari ya kuingiza mifugo ndani ya hifadhi ni kupata maradhi kwa wanyamapori wa hifadhi ama kusambaza magonjwa kwa wanyama waliopo nje ya hifadhi kikiwamo kimeta.

Alisema mbali na changamoto hiyo kumekuwa na tatizo jingine la uvunaji haramu wa samaki katika hifadhi kinyume cha sheria za hifadhi.

Alisema njia mbadala ya kuzuia uvuvi haramu wa samaki ni wananchi kutengenezewa mabwawa ili waache kuvuna samaki.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema wanachokifanya ni kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na uhifadhi ili wananchi waelewe umuhimi wa hifadhi.

Alisema wananchi hao wanatakiwa kujua mwingiliano wa wanyama kwenda kwenye hifadhi kunaweza kusababisha magonjwa.

"Mwingiliano ukitokea basi ni madhara kwa hifadhi na kwa mifugo ambayo inaingizwa katika hifadhi, kikubwa tunachokifanya ni elimu unajua mnyama hana mipaka ingawa hifadhi zina mipaka," alisema.



Mchonga vinyago akichora sehemu ya mbao iliyokatwa maalumu kwa ajili ya kutengenezwa kinyago. Aina hizo za mbao zinatokana na miti iliyoko katika misitu ya kupandwa Wilaya ya Mufindi mkoani Njombe. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Kigwangalla aitaka benki ya NCBA kuchochea utalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, ameitaka Benki ya NCBA kusaidia ustawi wa shughuli za utalii nchini kwa kutoa mikopo ya riba nafuu na kuahirisha ulipaji wa mikopo kwa watoa huduma wa shughuli za utalii, ili kuchochea ukuaji wa sekta hiyo.

Dk. Kigwangala alitoa rai hiyo, mwisho mwa wiki jijini Arusha, wakati akizindua matawi mawili mapya ya benki ya NCBA, ambayo ni Tawi la Clock Tower lililopo Fire Road, jengo la TFA na Tawi la Sokoine lililopo barabara ya Sokoine, Central Plaza ghorofa ya chini.

"Changamoto zozote zinazoikumba sekta ya utalii zina athari kubwa kwa sekta nyingine zote za uchumi wa mkoa huu. Hapa Arusha, utalii ukipiga chafya, mji mzima unapata mafua na utalii wa Arusha ukipata mafua, basi hali ya utalii nchini kote huambukizwa homa na ni kwa sababu asilimia kubwa ya watalii wanaokuja nchini hutembelea vivutio vinavyopatikana katika ukanda huu wa kaskazini, tunaamini ujio wa benki hii utakuwa na manufaa makubwa," alisema Dk. Kigwangala.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta, alisema wana fursa kubwa za uwekezaji katika kilimo na biashara za mazao ya chakula, kilimo cha bustani na ufugaji kwa ajili ya usalama wa chakula, matumizi ya viwandani na kuuza nje hufanywa ambazo benki hiyo inaweza kuwekeza.

"Ni matumaini yangu, benki ya NCBA imejizatiti kuwainua wakulima katika wigo mzima wa mnyororo wa thamani wa kilimo, kutoka mashambani hadi viwandani. Hii itabadilisha sekta hii muhimu ya uchumi kwa mkoa ili faida zinazopatikana ziifikie jamii na watu binafsi. Bila shaka, hauwezi kuutaja mkoa wa Arusha bila kuzungumzia utalii ambao unachangia zaidi ya asilimia 17 kwenye Pato la Taifa," alisema Kwitega.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NCBA, Margaret Karume, aliwashukuru wenyeji wa mkoa huo kwa kukubali mwaliko wao katika hafla hiyo na kuahidi kushirikiana na serikali katika safari ya kihistoria ya mafanikio.

"Tutafikia malengo yetu kwa kutoa huduma na bidhaa mbalimbali zitakazowezesha wateja wetu wa mashirika na wateja binafsi kufanikiwa zaidi kwenye mipango yao. Hii, kwa upande mwingine, itasaidia kufikia matarajio ya ukuaji wa uchumi nchini, Benki ya NCBA inathamini uhusiano na wateja wetu, na utoaji wa huduma bora kwa kiwango cha kimataifa kwa kuwa ndio kiini cha kila kitu tunachokifanya," alisema Karume.

## HABARI KIMATAIFA



Jengo la Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda, likiwaka moto usiku wa kuamkia jana. **PICHA: BBC**

# Moto wateketeza jengo Chuo Makerere

**Kampala,** Uganda

POLISI nchini Uganda wanachunguza chanzo cha moto uliokiteketeza chuo kikuu maarufu Makerere ambacho ni kikubwa na cha zamani zaidi kilichopo katikati mwa mji mkuu wa Kampala.

Taarifa za awali zinaonyesha kuwa huenda moto huo ulianzia kwenye paa na baadaye kusambaa kwenye sakafu za majengo ya vitengo vya fedha na rekodi za chuo.

Mwandishi wa BBC mjini Kampala anasema kuwa maofisa walikabiliana na moto mkubwa kuanzia takriban saa sita usiku hadi asubuhi Jumapili.

**Maofisa walikabiliana na moto mkubwa kuanzia takriban saa sita usiku hadi asubuhi Jumapili.**

Jengo hilo maarufu lililoungua ambalo linafahamika kama Ivory Tower, lenye kuta nyeupe na madirisha ya bluu, ni moja ya majengo yanayotambulisha chuo hicho maarufu barani Afrika.

Picha katika baadhi ya mitandao ya kijamii ya chuo hicho zinaonyesha sehemu ya nje ya kuta nyeupe za chuo hizo zilizoungua na kugeuka kuwa rangi nyeusi, na baadhi ya madirisha yaliyoungua:

Ivory Tower pia lina Ofisi ya Naibu Kansela wa chuo hicho pamoja na ukumbi mkuu wa chuo.

Naibu Kansela, Profesa Barnabas Nawangwe, kupitia akaunti yake ya mtandao wa Twitter, ameelezea tukio hilo kama asubuhi nyeusi sana na akaongeza kuwa uharibifu uliotokea ni wa kiwango cha kutoaminika:

Makerere ni mojawapo ya vyuo vikuu vya hali ya juu zaidi barani Afrika na ndicho chuo kikuu cha zamani zaidi katika Afrika Mashariki, kilianzishwa mwaka 1922 mara ya kwanza kama shule ya ufundi.

Viongozi mbalimbali wa Afrika, wamepata elimu ya juu katika chuo hicho, akiwamo mwasisi wa Taifa la Tanzania hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. **BBC**

## Marekani: Vikwazo vya UN kwa Iran vitekelezwa upya

**New York,** Marekani

MAREKANI imetangaza kuwa vikwazo vya Umoja wa Mataifa (UN), dhidi ya Iran vimeanza tena kutekelezwa na kuahidi kuwaadhibu wale watakaovikiuka, hatua ambayo inatishia Marekani kuendelea kutengwa na kuanza mivutano ya kimataifa.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Mike Pompeo, alisema serikali yake inakaribisha vikwazo vyote vilivyokuwa vimewekwa dhidi ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran. Kulingana na yeye, vikwazo hivyo vilianza kutekelezwa saa sita usiku wa kuamkia jana.

Serikali ya Rais Donald Trump, pia imeahidi kuliwekea vikwazo taifa lolote mwanachama wa UN, ambalo halitatekeleza vikwazo hivyo dhidi ya Iran. **DW**

## Kiongozi upinzani ashtakiwa ugaidi

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

ETHIOPIA imemfungulia mashtaka kiongozi wake maarufu wa upinzani, Jawar Mohammed, na watu wengine 23 kwa makosa yanayohusiana na ugaidi, ulaghai wa mawasiliano ya simu na uhalifu mwingine.

Kama watapatikana na hatia, huenda wakakabiliwa na kifungo cha maisha gerezani.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, imetangaza kuwa washtakiwa watafikishwa mahakamani leo, Jumatatu.

Mashtaka hayo yanatokana na machafuko makubwa yaliyozuka Julai katika maeneo ya mji mkuu Addis Ababa na Jimbo la Oromia baada ya kuuawa kwa mwanamuziki Hachalu Hundessa, ambaye alikuwa maarufu katika maandamano ya kuipinga serikali yaliyomwingiza madarakani Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, mwaka wa 2018. Serikali ilisema zaidi ya watu 180 waliuawa katika vurugu hizo za Julai. **DW**

## Kifurushi cha sumu kwenda kwa Trump chashtukiwa

**WASHINGTON,** Marekani

KIFURUSHI kilichokuwa na sumu ya ricin ambacho kilikuwa na anwani ya Rais wa Marekani, Donald Trump, kimezuiwa kabla ya kufika katika White House, maofisa wameviambia vyombo vya habari vya Marekani.

Barua hiyo iligunduliwa katika kitengo cha ukaguzi wa vifurushi vya barua katika Ikulu ya White House mapema wiki hii, wanasema maofisa. Walisema kuwa sumu hiyo iliyopatikana ndani ya bahasha ilitambuliwa kama ricin, sumu ambayo kwa kawaida hupatikana katika maharagwe.

Utawala wa Trump haujasema lolote kuhusiana na taarifa hiyo.

FBI pamoja na huduma za upepelezi wa siri wanachunguza kubaini ni wapi kifurushi hicho kilitoka na iwapo vifurushi vingine vya aina hiyo vilitumwa kupitia mifumo ya posta ya Marekani.

Polisi ya Canada-The Royal Canadian Mounted Police (RCMP) ilisema Jumamosi kuwa inashirikiana kwa pamoja na FBI kuchunguza barua "inayoshukiwa iliyotumwa katika ikulu ya White House".

Ricin hutengenezwa kwa kusindikwa kwa maharage ya castor. Ni sumu inayoua ambayo kama ikimezwa, kuivuta wakati wa kupumua au kuchomwa sindano yake, inaweza kusababisha kizunguzungu, kutapika, kuvuja damu ndani ya mwili na kusimamisha utendaji wa viungo vya ndani ya mwili.

Iwapo mtu atatumia sumu ya ricin, kifo chake kinaweza kutokea katika kipindi cha saa 36 na 72, kulingana na kiwango cha dozi iliyoingia mwilini mwake, kwa mujibu wa Kituo cha Marekani cha kudhibiti na kuzuwia magonjwa (CDC).

CDC kinasema sumu hiyo ambayo imekwishawahi kutumiwa katika njama za ugaidi, inaweza kutengenezwa kuwa silaha katika muundo wa poda, au mvuke.

White House na majengo mengine ya serikali kuu ya Marekani yaliwahi kulengwa kwa kutumia sumu ya aina hiyo miaka iliyopita. **BBC**

## Wapiganaji 30 wa Taliban wauawa

**KABUL,** Agfhanistan

JESHI la angani la Afghanistan, limefanya mashambulizi kadhaa kwenye ngome za Taliban na kuwaua zaidi ya wapiganaji 30 wa kundi hilo, wakati Rais Ashraf Ghani kwa mara nyingine akitoa wito wa kusitishwa mapigano.

Taliban imesema shambulizi hilo liliwaua zaidi ya raia 23 wakiwamo wanawake na watoto katika tukio hilo la karibuni nchini Afghanistan, ambalo limetokea hata wakati mazungumzo ya amani yakiendelea nchini Qatar.

Wizara ya Ulinzi, imesema wanamgambo wa Taliban walivishambulia vituo vya jeshi la Afghanistan katika eneo la Khan Abad mkoani Kunduz, kabla ya wanajeshi kujibu mashambulizi kwa mujibu wa taratibu za mapigano na kuwaua wapiganaji hao wa Taliban, wakiwamo makamanda wawili.

Katika taarifa, Taliban imekanusha kuwa wapiganaji wake walishambuliwa na kusema raia 23 waliuawa. **DW**

# BALE ATAKA MOLARI YA KUSHINDA MATAJI SPURS




**LONDON,** England

GARETH Bale anataka molari ya ushindi aliyoipata kule Real Madrid kuileta Tottenham Hotspur na kuisaidia klabu hiyo kumaliza ukame wa kutwaa mataji.

Tottenham ilitangaza Jumamosi kuwa Bale amerudi klabuni hapo kwa mkopo mrefu wa msimu mmoja akitokea Madrid, ambako alijiunga nao akitokea Spurs mwaka 2013 kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 85.

Kwa kipindi cha misimu yake saba aliyokaa Santiago Bernabeu, winga huyo mwenye umri wa miaka 31 ameshinda mataji ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne na mawili ya LaLiga.

Spurs imetwaa taji moja tu la ELF msimu wa 2007/08 kwa kipindi cha miaka 20 na Bale, ambaye anatarajiwa kuwa fiti na kuanza kucheza Oktoba baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, ana matumaini ya kumaliza ukame huo chini ya Kocha Jose Mourinho.

"Ni jambo zuri kurudi hapa. Klabu maalum kwangu, ndiko ambako nilitengeneza jina langu. Klabu yenye mashabiki wa aina yake, nina furaha kubwa kuwa hapa," alisema Bale akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Matumaini yangu sasa naweza kuwa fiti na kuisaidia timu kushinda mataji kwani naona ari ni kubwa.

"Kwa kwenda Madrid, ambako nimeshinda mataji mengi, nahisi ile morali ya namna ya kushinda nitaileta hapa."

# Neville afunguka upungufu Man United

**MANCHESTER,** England

GARY Neville amewaonya Manchester United wanahitaji mlinzi mpya wa kati kuliko wanavyomhitaji, Jadon Sancho baada ya kuanza vibaya msimu mpya wa Ligi Kuu England.

Nahodha huyo wa zamani wa United amesema kikosi cha sasa hakina nafasi ya kushinda taji la Ligi Kuu England kwa kuwategemea Harry Maguire na Victor Lindelof kwenye moyo wa ulinzi.

Kauli yake hiyo imekuja baada ya kikosi hicho cha kocha Ole Gunnar Solskjaer kuchezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Crystal Palace pale Old Trafford kwenye mchezo uliofanyika juzi usiku.

Baada ya kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England msimu uliopita, huku ikicheza mechi 14 katika mashindano yote bila kufungwa, United ilianza msimu huu 2020/21 kwa matumaini makubwa ya kumaliza kwenye nafasi nzuri.

Wamekuwa wanawania kutaka kumsajili winga wa Borussia Dortmund, Sancho klabuni hapo, lakini Neville amesema kipaumbele kwa sasa kinatakiwa kuangaliwa kwenye nafasi ya ulinzi.

Akizungumza na Sky Sports, Neville alisema: "Unaweza kuzungumza kuhusu Jadon Sancho vyovyote unavyotaja, lakini unatakiwa kwanza kupata mlinzi wa kati na bila hivyo huwezi kushinda taji la ligi.

"Hawataweza kushinda taji la ligi kwa safu ya ulinzi waliyonayo sasa. Wana walinzi ambao utawala wao na kazi yao ni ndogo, hivyo Lindelof na Maguire wanahitaji mtu wa kuwasaidia."

United ilianza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu England ikiwa ni wiki tano tangu kumalizika kwa msimu wa Europa Ligi 2019-20 ambapo walifungwa kwenye nusu fainali na Sevilla ambao ndio waliiibuka kuwa mabingwa wa michuano hiyo.





# *Ancelotti akunwa na kiwango Everton*

**LONDON,** England

CARLO Ancelotti amebainisha "ni wakati mzuri" kwa Everton baada ya Dominic Calvert-Lewin kufunga mabao matatu 'hat-trick' na James Rodriguez kufunga moja kwenye ushindi wa magoli 5-2 dhidi ya West Brom.

Kocha huyo wa zamani wa Milan na Real Madrid aliiongoza Everton kwenye mchezo huo wa pili wa Ligi Kuu England na kuondoka na pointi tatu wakati West Brom wakimpoteza Kieran Gibbs kwa kadi nyekundu.

Everton sasa ina pointi sita baada ya kuanza ligi kwa kuifunga Tottenham - na sasa wanaonyesha ishara kwamba watamaliza kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo kutoka ile nafasi ya 12 msimu uliopita.

Ancelotti aliiambia BT Sport alifurahishwa na upatina wa Calvert-Lewin na fowadi wa Brazil, Richarlison, akiongeza kwamba, James, alikuwa akiwasaidia wawili hao kwa karibu na "anafanya vizuri" baada ya kutua hapo kutoka Real Madrid.

"Nimeona ari na hamasa kubwa, hivyo wakati huu ni mzuri sana, lakini lazima tuwe makini kwa sababu kila mchezo ni mgumu," amesema raia huyo wa Italia.

James ameonyesha ishara nzuri katika siku zake mwanzo kabisa pale Everton, akifunga bao la pili dhidi ya West Brom, na Ancelotti akasema: "Anaufanya mchezo wa soka kuwa rahisi. Ameanza vizuri sana. Nina furaha kubwa kwa hili.

# DIOGO JOTA ATUA RASMI LIVERPOOL



**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imekiimarisha zaidi kikosi chake kwa kumsajili mshambuliaji wa Wolves, Diogo Jota kwa ada iliyoripotiwa ya pauni milioni 45.

Jota mwenye umri wa miaka 23, amesaini mkataba wa muda mrefu na mabingwa hao wa Ligi Kuu England, ambao pia walithibitisha ujio wa Thiago Alcantara kutoka Bayern Munich, Ijumaa iliyopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ataongeza uimara kwenye safu ya ushambuliaji ya Kocha Jurgen Klopp, ingawa anatarajiwa kuwa nyuma ya Mohamed Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino.

Jota ametua kwenye dimba la Anfield baada ya kuwa na misimu mitatu ya mafanikio ndani ya Wolves, klabu aliyojiunga nayo awali kwa mkopo kutoka Atletico Madrid mwaka 2017.

"Kwa hakika ni wakati mzuri zaidi kwa upande wangu na familia yangu," alisema Jota akiiambia tovuti ya Liverpool.

"Malengo yangu tangu nikiwa mtoto ni kujiunga na kubwa kama Liverpool - mabingwa wa dunia, ni ndoto iliyotimia. Nasubiria tu kuanza kucheza.

"Ni moja ya timu bora duniani, ni bora kwa wakati huu kwa sababu ni mabingwa wa dunia. Ukiangalia kwenye Ligi Kuu, mara zote unaiona Liverpool kama moja ya timu kubwa nchini, hivyo haikuwezekana kusema hapana."

# Reguilon nyota mpya Spurs akitoka Madrid

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur imethibitisha kumsajili, Sergio Reguilon kutoka Real Madrid.

Mlinzi huyo wa kushoto aliwasili katika kikosi hicho kinachonolewa na Kocha Jose Mourinho, Jumamosi.

Reguilon alinga'ara wakati akicheza kwa mkopo kule Sevilla msimu uliopita na kuwasaidia kutwaa taji la Ligi ya Europa na kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa LaLiga. Kiwango hicho kilimsaidia Reguilon kuitwa kwa mara ya kwanza kuichezea Timu ya Taifa ya Hispania mapema mwezi huu, wakati ripoti zilipokuwa zinamhusisha kuwaniwa na Manchester United, Chelsea na Paris Saint-Germain.

Hata hivyo, Tottenham imefanikisha dili la kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, ambapo ada yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 32.

Akiwa ni zao la akademi ya kulea vipaji ya Madrid, Reguilon ameondoka Santiago Bernabeu akiwa amecheza mechi 22 kwa kikosi cha kwanza, zote katika msimu wa 2018/19.

Sevilla walikuwa wanataka kumsajili moja kwa moja mlinzi huyo, lakini walishindwa na badala yake wakamsajili Marcos Acuna kutoka Sporting CP ya Ureno.







# Kocha Zidane hajui Hazard atarudi lini

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane hajui wakati gani Eden Hazard atakuwa fiti kuichezea Real Madrid wakati nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji akiendelea kuwa katika wakati mgumu hapo kwenye mji mkuu wa Hispania.

Ingawa Madrid walifanikiwa kutawala ligi na kutwaa taji la LaLiga kutoka Barcelona msimu uliopita, ulikuwa wakati mgumu zaidi kwa Hazard ambaye alitua hapo kwa ada ya awali ya euro milioni 100 kutoka Chelsea.

Alianza vizuri, lakini mambo yalikuwa magumu baada ya kufanyiwa operesheni ya mguu wa kulia uliovunjika.

Hazard mwenye umri wa miaka 29 alikwenda kwenye mechi za kimataifa wakati wa mashindano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya Denmark na Iceland, lakini hakucheza hata kwa dakika moja na ripoti kutoka Madrid zilidai mchezaji huyo alirudi kwenye mazoezi ya maandalizi ya msimu mpya akiwa ameongeza uzito.

Kabla ya timu yake kuanza kutetea taji lake dhidi ya Real Sociedad jana Jumapili, Zidane alithibitisha Hazard kutocheza mchezo huo.


"Siwezi kuwaambia ni lini atakuwa tayari kurudi uwajani, bado anaendelea kujipambania," alisema.

"Jambo la msingi ni namna gani mchezaji anajisikia. Tunatakiwa kujiandaa kwa ajili ya msimu.

"Jambo pekee ambalo anatakiwa kufanya ni kuwa fiti kwa asilimia 100 na kurudi kufanya kazi yake."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AMPIGIA HESABU LACAZETTE

## ●●● Kocha huyo aweka wazi bado Arsenal haijaanza mazungumzo ya kumpa mkataba mpya...

**LONDON,** England

ARSENAL bado haijaanza mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na Alexandre Lacazette, kocha wa timu hiyo, Mikel Arteta amethibitisha.

**Mkataba wa sasa wa Lacazette na klabu hiyo ya Ligi Kuu England unamalizika mwaka 2022, lakini kumekuwa na uvumi kuhusiana na majaliwa ya fowadi huyo klabuni hapo yapo shakani.**

Raia huyo wa Ufaransa alifunga bao lake la 50 kwa Arsenal wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya West Ham, Jumamosi kwenye mchezo wa Ligi Kuu England kwenye Uwanja wa Emirates.

Lakini bado hakujakuwa na mazungumzo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kuhusu kuongeza mkataba wake hapo Arsenal.

Awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kujiunga na klabu ya Atletico Madrid, mpango unaoonekana kwamba ulishindikana.

Pia mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Juventus nao walitajwa wana nia ya kumsajili mchezaji huo, lakini ripoti za baadaye zinasema kibibi kizee hicho cha Turin hakina mpango huo.

Na sasa Arteta amebainisha kwamba, Arsenal bado haijafanya lolote katika kuhakikisha wanaongeza mkataba wa nyota huyo, kwani hakuna kilichozungumza hadi sasa.

"Kwa wakati huu, hatujaanza majadiliano ya kuhusu kumsainisha mkataba mpya," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo wa juzi Jumamosi.

"Tuna mambo mengi bado ya kufanya katika soko la sasa na kwa sasa tunakimbizana kwanza na mambo hayo."

Arteta alisema amefurahishwa na kiwango cha Lacazette, ambaye alijiunga na klabu hiyo akitokea Lyon ya Ufaransa mwaka 2017.

"Yeye ni mchezaji ambaye namfurahia kuwa kwenye kikosi changu. Nafikiri tumemwonyesha imani yetu tangu amewasili hapa," alisema.

"Lakini hatujaanza mazungumzo yoyote. Tunajua kwamba mchezaji yeyote ambayo yupo chini ya miaka miwili kwenye mkataba wake unatakiwa kuanza naye mazungumzo."

Arsenal imeanza vizuri zaidi msimu huu mpya wa Ligi Kuu England, ambapo katika mchezo wake wa ufunguzi dhidi ya Fulham ilishinda mabao 3-0 na juzi Jumamosi ikashinda 2-1 dhidi ya West Ham.

## ZISIKUPITE

### LINGARD ATAKIWA SPURS

TOTTENHAM inataka kumsajili kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard (27), kwa ada ya pauni milioni 30. ***(Daily Star Sunday)***

### CHELSEA KUMKOSA RICE

MABOSI wa West Ham wameiambia Chelsea kuwa kiungo wa Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 21, Declan Rice, hauzwi. ***(90min)***

### SEVILLA YAIGOMEA CITY

MANCHESTER City imewasilisha ofa ya pauni milioni 50.4 ili kumnasa beki Mfaransa, Jules Kounde lakini klabu ya Hispania ya Sevilla imekataa. ***(Marca)***

### MENDY RASMI CHELSEA

CHELSEA imefikia katika makubaliano na Rennes ya nchini Ufaransa kwa ajili ya uhamisho wa golikipa wa Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy (28), kwa ada ya pauni milioni 22. ***(Observer)***

### BARCA KIFUNGONI

BARCELONA imefungiwa kumsajili kiungo wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Georginio Wijnaldum (29), kwa sababu ya kukiuka kanuni za fedha zilizowekwa na wasimamizi wa La Liga. ***(Sunday Mirror)***

### CHAMBERLAIN SOKONI

WOLVES imeweka wazi inahitaji kumsajili kiungo wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Alex Oxlade-Chamberlain, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Sunday Mirror)***

### JAMES ANUKIA LEEDS

LEEDS United itajaribu kufanya mchakato wa kumsajili winga wa Manchester United, Daniel James (22), kama mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Wales ataonekana hana nafasi kwenye kikosi cha Old Trafford. ***(Daily Star Sunday)***

### VALENCIA YAMTAKA ROMERO

VALENCIA inajiandaa kutoa dau la pauni milioni sita ili kumsajili golikipa wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Argentina, Sergio Romero, ambaye ana umri wa miaka 33. ***(Sunday Mirror)***

### EVERTON YALAMBA DUME

KIUNGO mchezeshaji wa Everton, James Rodriguez (29), alihamia Real Madrid kama mchezaji huru, klabu ya zamani nyota huyo wa kimataifa, Banfield imesema. ***(Sunday Times - subscription required)***

### NDOMBELE KUBAKIA SPURS

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Tanguy Ndombele (23), ambaye anahusishwa na kujiunga na Inter Milan pamoja na Juventus, amefikia uamuzi wa kubakia Tottenham baada ya kumaliza tofauti zake na Jose Mourinho. ***(L'Equipe, via Football Italia)***

### KEAN KUREJEA JUVE

JUVENTUS inajipanga kumrejesha klabuni kwake straika wa Everton na Timu ya Taifa ya Italia, Moise Kean (20), kwa mkataba wa mkopo, lakini kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja hapo baadaye. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Viongozi wanawake watakiwa kujituma

**Na Frank Monyo**

WANAWAKE walioshiriki semina ya uongozi na utawala wa soka wametakiwa kutumia mafunzo waliyopewa ili kuinua mchezo huo kwa ujumla na si kwa ajili ya wanawake pekee.

Hayo yalisemwa juzi na Mkufunzi wa Kimataifa anayetambulika na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Dk. Henry Tandau, wakati wa ufungaji semina hiyo iliyoshirikisha washiriki 32 hapa jijini, Dar es Salaam.

Tandau alisema lengo la kufanyika kwa semina hiyo ni kuwapa uwezo wanawake kwa ajili ya kushiriki kuinua mchezo wa soka nchini.

Alisema wanawake kama wadau wa soka nchini wakijengewa uwezo, wana nafasi nzuri ya kuendeleza soka la wanawake na hata la wanaume.

"Sikufundisha uongozi na utawala wa mpira wa miguu kwa wanawake kwa ajili ya kusimamia wanawake tuu, ila kuzisimamia taasisi za mpira wa miguu ndani na nje ya nchi," alisema Dk. Tandau.

Kwa upande wa KCB, ambao ndiyo wadhamini wa mafunzo hayo, wameipongeza TFF kwa kubuni njia ya kuwainua wanawake katika utawala na uongozi wa mpira wa miguu na kueleza hiyo ni fursa muhimu kwao.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Wateja Wakubwa, Christina Manyenye, alisema washiriki wa mafunzo hayo wanatakiwa kutafuta fursa kama mafunzo waliyopata yalivyokusudiwa.

## Kidimni Queens yaingia 'mitini'

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kidimni Queens ilishindwa kutokea kuwakabili New Generation katika mechi ya ligi maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar iliyotarajiwa kuchezwa juzi jioni Visiwani hapa.

Hata hivyo, haikufahamika ni sababu gani zilipelekea timu hiyo kutofika uwanjani wakati ilishiriki kikamilifu katika kikao cha maandalizi ya mechi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Soka la Wanawake Zanzibar, Nasra Juma, alisema kamati yake itakutana leo ili kujadili suala hilo na kuchukua hatua kwa lengo la kuhakikisha kosa kama hilo halijirudii.

Nasra alisema viongozi wa timu hiyo walishiriki vikao mbalimbali vya maandalizi na kuthibitisha klabu yao itashiriki ligi licha ya kukabiliwa na changamoto za vifaa, lakini ikiwamo jezi na viatu ambavyo walipewa na shirikisho hilo.

"ZFF kupitia Kamati ya Soka la Wanawake iliandaa ligi ndogo ambayo inachezwa kwa mzunguko mmoja ili timu zipate kujitayarisha na ligi ya msimu mpya, makatibu wa timu zote walihudhuria vikao vyote, sasa inapotokea timu kutokuja uwanjani hii haileti taswira nzuri, kamati lazima tuchukue hatua za kinidhamu," alisema Nasra.

Alisema ligi hiyo itaendelea tena kwa Green Queens kuwakabili Women's Fighter mchezo utakaopigwa kwenye Uwanja wa Mau B kuanzia saa 10:00 jioni.

# NAMUNGO FC YAANIKA KINACHOWATESA BARA

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupoteza mchezo wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Namungo, Thierry Hitimana, alisema kinachoisumbua timu yake ni kukosekana kwa muunganiko mzuri wa wachezaji wapya na wa zamani.

**Namungo FC juzi ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wenyeji Tanzania Prisons, katika mchezo wa raundi ya tatu uliochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga mkoani Rukwa.**

Hitimana aliliambia gazeti alisema anasikitika kuona amepoteza pointi sita na makosa yanayofanywa na wachezaji wake yamekuwa yakijirudia.

"Wachezaji wamekuwa wakifanya makosa yale yale, na hali hii ya kurudia makosa inasababishwa na kutokuwa na muunganiko mzuri, ninaendelea kufanyia kazi ili kupata matokeo mazuri katika mechi zinazofuata," alisema Hitimana.

Aliongeza pia kikosi chake kinakabiliwa na majeruhi na kulazimika kutumia wachezaji wapya ambao bado hawako 'fiti' kupambana na ushindani wa ligi hiyo.

Aliwataja wachezaji ambao bado ni majeruhi ni pamoja na Haruna Shamte, Stephen Sey na George Manyanya.

"Kwa sasa napambana kukijenga kikosi changu maana huko mbele tunaelekea katika mashindano ya kimataifa, tunahitaji kuwa makini zaidi katika Ligi Kuu kabla hatujaanza kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Hitimana.

Alieleza tatizo lingine ni washambuliaji wake kutokuwa makini na kupoteza nafasi za kufunga zilizotengenezwa.

"Tumepoteza pointi nyumbani na ugenini, ukiangalia mechi, utaona tumepata nafasi nyingi ila hatukutumia vyema nafasi tulizopata, nimeanza kufanyia kazi kuhakikisha tunaingia imara zaidi tutakapocheza dhidi ya Mbeya City," alisema Hitimana.

Namungo FC itaifuata Mbeya City katika mechi ya raundi ya nne itakayochezwa Septemba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Biashara ya DCB walioshiriki mbio maalum za Masaki Corporate Marathon wakifanya mazoezi ya viungo baada ya kumaliza mbio hizo kwenye Uwanja wa The Green, Masaki jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Multichoice yaahidi makubwa nchini*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kampuni ya MultiChoice Tanzania ikibainisha mambo mbalimbali iliyofanya hapa nchini tangu kuanzishwa kwake zaidi ya miaka 20, ikiwamo kutoa ajira, kukuza tasnia ya filamu na sanaa imeahidi itaendelea kuwa kitovu cha burudani kitaifa na kimataifa kwa wateja wake wa DStv.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi jioni, Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, alisema kampuni hiyo imejipanga kuhakikisha kazi za wasanii wa hapa nchini zinafanya vyema na zinatayarishwa katika kiwango cha kimataifa.

Alisema miaka mnne iliyopita, MultiChoice ilianzisha chaneli maalum ya Maisha Magic Bongo ambayo ni mahsusi kwa maudhui ya ndani ili kutoa nafasi zaidi ya kuwatangaza wasanii wa Tanzania.

"Chaneli hii inabeba maudhui ya Kitanzania kwa asilimia 98, na maudhui haya huzalishwa hapa nchini na wazalishaji na waigizaji wa hapa nchini. Katika kipindi kifupi cha miaka minne, chaneli hii imetumia fedha nyingi kwa uzalishaji na ununuzi wa maudhui ya kitanzania na imefanya kazi na wazalishaji zaidi ya 200, waigiaji zaidi ya 2,000 na zaidi ya wasaidizi 5,000," alisema Jacqueline.

Katika kuimarisha tasnia ya filamu, Jacqueline alisema kampuni hiyo inashirikiana na bodi ya filamu katika kutoa mafunzo kwa wazalishaji hapa nchini, ambapo mwaka 2018 walifanya mafunzo katika mikoa mbalimbali na sasa wapo kwenye mazungumzo ya kushirikiana na bodi ya filamu kuendesha mafunzo mengine.

Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, alisema wamekuwa na ushirikiano mkubwa wenye tija kati yao na kampuni hiyo na ushirikiano huo umezaa matunda ya kusaidia kutoa ajira, mafunzo na kununua kazi za wasanii wa hapa nchini.

Msanii wa filamu, Jacob Steven 'JB' alisema kampuni hiyo imekuwa mkombozi kwa wasanii kiuchumi kwa sababu ya kununua kazi zao kwa wingi.

Kampuni hiyo imetajwa pia kushiriki kuitangaza Tanzania kwenye ramani ya michezo duniani ikiwamo kufanya kazi na watangazaji maarufu wa michezo ambao ni Aboubakar Lyongo, Maulid Kitenge na Oscar Oscar.

Michezo
Jumatatu Septemba 21, 2020
Nipashe




Arteta ampigia hesabu Lacazette UKURASA 22




Mshambuliaji wa Tottenham, Heung-min Son (kulia), akifunga bao huku golikipa wa Southampton, Alex McCarthy (katikati), akishindwa kuokoa shuti la Mkorea huyo katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa katika Uwanja wa St Mary's jana, mchana. Spurs ilishinda mabao 5-2. **PICHA: MTANDAO**

# Zlatko: Tatizo mabao kiduchu Yanga ni hili

## Asema ameanza kulifanyia kazi, kikosi chaingia kambini Dar leo kupewa mbinu za Mtibwa huku...

**Na Isaac Kijoti,** BUKOBA

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikiibuka na ushindi wa bao 1-0 kwa mara ya pili mfululizo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mserbia Zlatko Krmpotic, ametoa sababu ya matokeo hayo kiduchu huku akieleza tayari suluhisho la tatizo hilo analo.

**Juzi Yanga ikiwa ugenini katika Uwanja wa Kaitaba mjini hapa, ilishinda bao 1-0, kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar ikiwa ushindi huo ni wa pili mfululizo, lakini tangu kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu 2020/21, Yanga haijawahi kufunga zaidi ya bao moja kwenye mchezo mmoja.**

Katika mechi ya ufunguzi wa msimu huu dhidi ya Tanzania Prisons, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1 kabla ya kushinda 1-0 kwa mbinde dhidi ya Mbeya City katika mchezo uliofuata, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Lakini akizungumzia matokeo ya timu yake inayoyapata baada ya mechi ya juzi dhidi ya Kagera Sugar, Zlatko alisema anafahamu tatizo lilipo na tayari anaendelea kulifanyia kazi.

"Leo tumeshinda tena kwa goli moja na wapinzani wetu wameonyesha mchezo mzuri, lakini cha kushukuru tumepata pointi tatu ndicho kitu cha muhimu.

"Tatizo kubwa bado sijapata muunganiko mzuri wa timu, kadri tunavyoendelea natumaini nitaweza kuiunganisha na timu kucheza vizuri na kufunga mabao mengi," alisema Zlatko ambaye alichelewa kujiunga na timu hiyo, hivyo kukosa muda wa maandalizi ya msimu mpya.

Kuhusu mechi inayofuata, Zlatko alisema, ushindi huo utawapa hamasa ya kufanya vizuri tena ugenini wakati huu wakijiandaa kuifuata Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro mwishoni mwa wiki. Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, mbali ya kuwapongeza wapinzani wao kwa ushindi huo, alisema mechi ilikuwa nzuri kwa pande zote, lakini hawana budi kwenda kufanyia kazi makosa waliyofanya kwa ajili ya mchezo ujao.

"Ndiyo kwanza mwanzo wa ligi, michezo bado ipo mingi, tutaenda kujipanga zaidi kwa ajili ya mechi zijazo," alisema beki na nahodha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Kuhusu anayepaswa kubebeshwa lawama kwa bao hilo pekee la dakika ya 72 lililofungwa na Tonombe Mukoko akiitendea haki krosi ya Tuisila Kisinda, Maxime alisema hakuna wakulaumiwa.

"Wenzetu walikuwa imara zaidi kwenye kuzuia na kuhusu bao hilo, huwezi kumlaumu mchezaji yeyote kwa sababu ulipigwa mpira mrefu, mabeki wetu wakazidiwa mbio na (Kisinda) akapiga krosi iliyomkuta mfungaji," Maxime alisema.

Maxime ambaye kipindi chote cha dirisha la usajili alikuwa akihusishwa na kujiunga na Yanga kama kocha msaidizi, alisema bado hawajapata matokeo mazuri msimu huu, hivyo wanatarajia kujipanga kwa mchezo ujao dhidi ya KMC FC.

"Msimu huu tumeshacheza mechi tatu, na tumepoteza mbili na sare moja, hivyo mechi bado ni nyingi tunarejea kufanyia kazi kasoro zilizojitokeza katika mchezo huu kwa ajili ya mechi ijayo."

**Wakati huo huo**, baada ya kikosi cha Yanga kurejea jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema, wachezaji watarejea makwao kwa mapumziko kabla ya leo kuingia kambini tayari kwa maandalizi ya mchezo ujao.

"Timu imerejea leo (jana), na wachezaji kwenda kwao kwa mapumziko na kesho (leo), wataingia kambini tayari kujiandaa na mechi dhidi ya Mtibwa," alisema Bumbuli.

Yanga yenye pointi saba, itasafiri kuifuata Mtibwa Sugar katika mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili.

# Azam FC yaishusha Yanga kileleni

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee lililofungwa na Mnyarwanda Ally Niyonzima wa Azam FC katika mechi dhidi ya Mbeya City iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya jana, liliiondoa Yanga katika usukani wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kiungo huyo alisajiliwa msimu huu kutoka Rayon ya Rwanda, alifunga bao kwa kichwa dakika ya 24, akiunganisha mpira wa kona iliyochongwa na Never Tegere.

Kwa ushindi huyo, Azam imefikisha pointi tisa ikiwa imeshinda mechi zote tatu, ikiifunga Polisi Tanzania bao 1-0 na Coastal Union mabao 2-0 na kuiacha Yanga ikiwa na pointi saba ilizozipata kwa kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Prisons, ikishinda bao 1-0 dhidi ya Mbeya City na bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar Jumamosi iliyopita.

Mpaka sasa Azam imefunga mabao manne na haijaruhusu hata mara moja vyavu zake kutikiswa.

Ulikuwa ni ushindi wa kwanza pia kwa Azam ikiwa ugenini, ambapo ilibidi ipigane kufa na kupona kuzipata pointi hizo kwani wenyeji wao walicharuka dakika 15 za mwisho kwa mashambulizi mfululizo, lakini washambuliaji wake kina Siraji Juma, Abasalim Chidiebere hawakuwa makini.

Shambulio pekee la hatari zaidi lililofanywa na Mbeya City ilikuwa dakika ya 51, wakati Siraji Juma alipoupata mpira uliokuwa unazagaa kwenye lango la Azam, akaachia shuti kali lililogonga nguzo ya pembeni na kurejea uwanjani kabla ya kuokolewa na mabeki wa Azam, ambao walikaa imara kulilinda lango lao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >